**AJIRA** mpya kada afya sasa lazima kufanyiwa usaili

UKURASA 2

**SIMBA** yatikisa kwa magoli ya vichwa Ligi Kuu

UKURASA 14



**BIL. 600/-** kutumika kulinda afya ya mama na mtoto

UKURASA 18


Spotika

ANAPOWEZA KUCHEZEA CHIESA KIKOSI CHA LIVER

ISIKUPITE

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Septemba 2, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581787

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Wananchi watinga polisi msako mama aliyetoweka 1992

UKURASA 2




Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Samia Suluhu Hassan akizindua kitabu cha miaka 60 ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Majeshi, Jenerali Jacob Mkunda. **PICHA: IKULU**

# Samia ajivunia mafanikio lukuki miaka 60 ya JWTZ

UKURASA 2



UKURASA WA 6

## KILIO UPANGAJI MATOKEO SI SUALA LA KUSUBIRI KANUNI

BAADA ya wadau wengi wa soka kupiga kelele ya kuwa na mdhamini anayedhamini klabu zaidi ya moja kwenye Ligi Kuu, Bodi ya Ligi...

UKURASA WA 17

## MATUKIO 165 YA UKATILI, UDHALILISHAJI YARIPOTIWA ZANZIBAR

MATUKIO 165 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa visiwani Zanzibar katika kipindi...

## Ulimwengu: Vyombo vya habari viweke wazi ukweli kwa maslahi ya nchi

UKURASA 4

**MICHEZO** IBENGE: SIMBA NI SIMBA TU, ITATISHA UK 24

MAONI, KATUNI UK.6

# Ajira mpya kada ya afya sasa lazima usaili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAOMBAJI takriban 37,534 wa nafasi za kazi za kada ya afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa leo wanaanza kufanyiwa usaili katika vituo vilivyoko mikoa husika.

Julai 7, 2024, serikali ilitangaza nafasi za kazi 9,483 za sekta ya afya. Awali kada hizo pamoja na ualimu waombaji walikuwa wakiomba kupitia mfumo wa ajira wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na hakukuwa na usaili wa aina hiyo.

Waombaji walikuwa wakiomba kupitia mfumo huo na baada ya uchambuzi wa waombaji wenye sifa, walikuwa wanapangiwa vituo vya kazi moja kwa moja.

Hivi sasa nafasi hizo za ajira, usaili unafanywa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Katika tangazo lililotolewa na sekretarieti hiyo la kuwaita kwenye usaili waombaji, mnabainishwa kuwa usaili huo utaendeshwa kuanzia Septemba 2 hadi 12 mwaka huu.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu alisema kuwa azma ya serikali ya kupeleka kibali cha ajira kwa kada za afya na elimu katika Ofisi ya Rais - Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni kuhakikisha serikali inapata watumishi wenye sifa ili kuongeza tija na ubora katika utumishi wa umma.

Sangu, akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kibali cha ajira mpya kwa mwaka wa fedha 2023/24 mbele ya Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, alisema Sekretarieti ya Ajira tayari imefanya jitihada kubwa katika kufanyia kazi kibali hicho.

Alisisitiza kuwa zoezi la usaili litaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

Awali akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kibali hicho, Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Samwel Tanguye, alisema sekretarieti hiyo imeshachakata maombi yote yaliyotumwa kwa kada za afya na elimu na kuwapata waombaji waliokidhi vigezo na tayari kwa kada za afya wameshaitwa kwenye usaili unaotarajiwa kuanza Septemba 2, 2024.

"Kwa wale ambao hawakuitwa kwenye usaili wamepewa sababu kupitia kwenye akaunti zao walizotumia kuwasilisha maombi yao ya kazi (Ajira Portal)," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Florent Kyombo, alipongeza sekretarieti hiyo kwa ubunifu na uwajibikaji mkubwa katika kutekeleza majukumu yake.

Mjumbe wa kamati hiyo, Yahaya Masare, alisema amefurahishwa na uamuzi wa kuhakikisha usaili unafanyika katika ngazi ya mikoa kwa kada za afya na ualimu.

Kwa mujibu wa vipeperushi vya sekretarieti hiyo, wasailiwa wa ngazi ya shahada watafanya usaili kidigitali (OATS), wenye stashahada na astashahada watafanya kwa njia ya kuandika kawaida.

Vilevile, kwa usaili wa kuandika, mchujo utafanywa katika mkoa ambao msailiwa anaishi kwa sasa na usaili wa mahojiano ya ana kwa ana utafanyika katika mkoa ambao mwombaji ameainisha kwenye maombi ya kazi (mkoa aliojaza kwenye barua ya maombi ya kazi kama kipaumbele chake cha kupangiwa kazi).



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Cane Growers wakionyesha maboksi ya pedi za kike zilizotolewa na Kampuni ya Kilombero Sugar jana, wilayani Kilombero. Mchango huo ni sehemu ya mpango wa kukomesha changamoto ya hedhi salama kwa wanafunzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia ajivunia mafanikio lukuki miaka 60 ya JWTZ

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema katika miaka 60 ya utendaji wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), limefanya mambo makubwa, ikiwamo kudumisha ulinzi na amani ya nchi.

Amesema ufanisi huo umetokana na jitihada za jeshi hilo kutekeleza kwa vitendo wosia wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliotoa wakati analihutubia kwa mara ya kwanza, akisisitiza "moyo kwanza kabla ya silaha".

Alisema mwasisi huyo pia alilisitiza kulinda katiba na uhuru wa nchi, kufanya mafunzo na mazoezi ili kujiweka tayari kivita wakati wote, kufundisha umma shughuli za ulinzi, kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kutoa misaada ya kibinadamu na uokoaji wakati wa maafa na kushiriki ulinzi wa amani na ukombozi.

Rais Samia aliyasema hayo jana Dar es Salaam aliposhiriki Kilele cha Miaka 60 ya jeshi hilo kilichohudhuriwa na viongozi wakuu wa nchi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Rais Samia alisema anafurahi kuona kuwa tangu kuanzishwa kwake miaka 60 iliyopita, jeshi hilo limetekeleza majukumu hayo kwa ustadi mkubwa.

Alitaja mafanikio hayo kuwa ni kulinda uhuru, katiba na mipaka ya nchi hiyo ardhini, angani na majini ikiwamo kuzima matukio makubwa yanayotishia uhuru na umoja wa nchi.

Alisema jeshi hilo pia limelinda na kuenzi Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na Mapinduzi ya Zanzibar, kushiriki na kufanikisha harakati za ukombozi katika Bara la Afrika, na baada ya ukombozi jeshi hilo limeendelea kushiriki kikamilifu na kwa mafanikio makubwa kwenye operesheni za kulinda amani kwa nchi kama Liberia, Sudan, Lebanon na Ivory Coast.

"Lakini jeshi letu pia linafanya kazi ya kulea vijana wa Tanzania kwa kuwafundisha uzalendo na maadili na kujitegemea kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)," alisema.

Kwa mujibu wa Amiri Jeshi Mkuu, jeshi hilo pia linatoa huduma za afya na elimu kupitia hospitali walizojenga pamoja na vyuo ikiwamo Chuo cha Taifa cha Ulinzi.

Alisema jeshi hilo limeendelea kuwa jeshi la ulinzi na si la uvamizi kwa kuwa halijawahi kuvamia nchi yoyote na wala halina mpango huo.

Pia alisema limekuwa mstari wa mbele kutoa misaada ya huduma pale wananchi wanapokabiliwa na majanga ya asili au ajali, akitaja mfano mmoja wapo kuwa ni namna lilivyojitoa kuwasaidia wananchi wa Hanang' walipovamiwa na maporomoko ya tope na Malawi mwaka 2023.

Alisema limekuwa kinara katika kutafsiri dira, sera na mipango ya serikali katika awamu zote za uongozi, ikiwamo vita dhidi ya ujinga, maradhi na umaskini kupitia mafunzo wanayotoa katika taasisi zao.

"Jeshi letu pia hivi karibuni wametekeleza miito yote inayotolewa na serikali.

Kwa mfano, limeshiriki vyema na kwa ufanisi mkubwa ujenzi wa Ikulu yetu mpya Chamwino, Dodoma na ukuta wa Mirerani wenye urefu wa kilomita 24.5 ikiwa ni moja ya ulinzi wa rasilimali madini," alisema.

Katika kutekeleza kaulimbiu 'Kazi Iendelee', Rais Samia alisema jeshi hilo linajielekeza katika mageuzi ya mifumo ya ulinzi na uchumi duniani, ukiwamo utekelezaji mkakati wa taifa wa kuimarisha uchumi na upatikanaji fedha za kigeni kwa kuzalisha bidhaa mbadala zinazoagizwa kutoka nje na kuimarisha uwekezaji, hivyo limeanza kuhuisha na kuimarisha viwanda vyake.

Rais alisema ameshuhudia jeshi hilo likiwachukilia hatua bila kuchelewa maofisa wanaokwenda kinyume cha misingi mikuu ya utumishi, ili kuendeleza nidhamu na utiifu katika jeshi na nchi.

Rais Samia alishukuru makamanda na wapiganaji wote wa jeshi hilo kwa kuendelea kuwa na moyo wa kizalendo na kutii viapo vyao na kuwa Watanzania wanathamini kazi wanayofanya katika nchi.

"Mimi binafsi kama Amiri Jeshi Mkuu, kila ninapotembelea au kushiriki shughuli za jeshi letu, ninashuhudia utayari, uhodari, umahiri na ujasiri wa jeshi hili, na huwa ninaridhika kuwa jeshi letu lipo katika kiwango cha juu na ninapata matumaini makubwa kwamba kesho ya nchi na watoto wetu ipo salama," alisema.

Rais Samia aliwasihi wananchi kuendelea kutimiza wajibu wao wa kikatiba Ibara ya 28(1) kwa kulinda amani ya nchi yao na kuwakemea wanaochochea uhasama na uvunjifu wa amani.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stargomena Tax, alisema kuwa JWTZ liko imara, weledi na mafanikio makubwa kwa kipindi kirefu, ni zao la uongozi mahiri, maono sahihi, mipango mizuri ya taifa na uhodari, utiifu na uzalendo wa hali ya juu ya viongozi wa taifa hilo.

Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, alishukuru serikali kwa kuiunga mkono jeshi hilo, ukiwamo ununuzi wa zana za kisasa za kufanyia kazi ambazo zinarahisisha utekelezaji majukumu yao ili kuhakikisha mipaka ya nchi ipo salama.

## Dk. Mwinyi aona fursa Indonesia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameeleza fursa za ushirikiano na Indonesia yenye teknolojia za kisasa.

Amesema Zanzibar ina nafasi nzuri ya kujifunza mambo mbalimbali, ikiwamo kilimo na usarifu wa mwani, uchimbaji mafuta na gesi, utalii na bandari kwa Indonesia kutokana na uzoefu, mbinu na teknolojia waliyonayo hasa katika uchumi wa buluu.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati anafungua Jukwaa la Uwekezaji la Zanzibar - Indonesia 2024, ambalo limeandaliwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

Rais Dk. Mwinyi ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alieleza kufurahishwa na mwamko wa jukwaa hilo kwa kujitokeza kwa wingi wawekezaji ambao wameonesha nia ya kuwekeza Tanzania, ikiwamo Zanzibar.

"Hivyo, tutarajie wawekezaji mbalimbali, hususan katika sekta ya uchumi wa buluu kutoka Indonesia," alisema.

Jukwaa hilo la kimkakati limekutanisha viongozi wa juu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Indonesia, wakiwamo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Sharif Ali Sharif.

Pia wamo Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Indonesia, Pahala Mansury; Waziri wa Madini Tanzania, Anthony Mavunde; Balozi wa Tanzania Indonesia, Makocha Tembele pamoja na wafanyabiashara na wawekezaji.

Jukwaa hilo limelenga kukuza ushirikiano wa kiuchumi kupitia sekta ya uchumi wa bluu, ukiwamo utalii, bandari, mafuta na gesi, usafiri wa baharini, uvuvi na usarifu wa mwani.

Rais Dk. Mwinyi aliwasili Bali, Indonesia Agosti 31, 2024 kumwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Pili wa Jukwaa la Indonesia na Afrika 2024 unaotarajiwa kuanza leo.



Chifu wa Ukoo wa Wahejiu wanaotokana na kabila la Warimi, wilayani Ikungi mkoani Singida, Thomas Mgonto (katikati), akishiriki maadhimisho ya sikukuu ya kichifu yaliyofanyika Kata ya Siuyu, wilayani Ikungi mwishoni mwa wiki. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wananchi watinga polisi wakitaka ndugu aliyepotea miaka 32 atafutwe

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKATI matukio ya utekaji na watu kutoweka yakiripotiwa katika maeneo mbalimbali nchini, wakazi wa Kijiji cha Pugizi, wilayani Ikungi, mkoani Singida wametinga katika kituo cha polisi kuomba Jeshi la Polisi lisaidie kumtafuta ndugu yao aliyepotea katika mazingira yenye utata miaka 32 iliyopita.

Wananchi hao ambao ni ndugu wa Asha Salum Nzile, wamefika Kituo cha Polisi Singida Mjini na kufungua faili PHQ/SIN/IRA/7004/2024 la kupotelewa na ndugu yao aliyepotea katika mazingira ya kutatanisha mwaka 1992 katika Kijiji cha Pugizi, Kata ya Mwaru, Tarafa ya Sepuka, wilayani Ikungi.

Mtoto wa mama huyo aliyepotea, Salum Nzile, alisema kuwa tangu mama yake alipotoweka miaka 32 iliyopita, wamefanya jitihada kadhaa za kumtafuta bila mafanikio.

Alidai kuwa mara ya mwisho walipomwuliza mjomba wao aliyemtaja kwa jina la Jumanne Salum, aliwaeleza kuwa Asha (aliyepotea) amempeleka mkoani Tabora.

Alisema baada ya kuelezwa hivyo na mjomba wao huyo, alikwenda hadi Tabora kumtafuta mama yake bila mafanikio na baadaye mwaka huu, wamefanya kikao cha familia kujadili aliko Asha.

Salum alidai kuwa katika kikao hicho, mjomba wake alithibitisha kusema uongo kwamba Asha yuko Tabora na baadaye alikubali kutoa mali zilizoachwa na mama huyo; ng'ombe 10 na ekari 10 za shamba, zote walikabidhiwa Mei mwaka huu.

Alisema makabidhiano ya mali hizo yalifanyika kwa kuandikishana katika ofisi ya kijiji chini ya usimamizi wa Ofisa Mtendaji wa Kijiji na Mwenyekiti wa Kijiji.

Hata hivyo, alisema kuwa katika hali ya kushangaza, taarifa ya makabidhiano ya mali hizo ambayo ni ya maandishi kama ushahidi, inadaiwa kupotea katika mazingira yenye utata kabla hajapewa nakala katika Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji cha Pugizi.

Alidai kuwa kupotea kwa taarifa hiyo kunamtia wasiwasi kwamba huenda kuna mchezo mchafu unataka kufanyika anyang'anywe mali hizo, hivyo akaamua kulifikisha suala hilo kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ambaye aliamuru iandikwe taarifa nyingine, lakini hadi sasa hakuna utekelezaji.

Rajabu Mrisho, maarufu Kayanda, kaka wa Asha (aliyepotea) alisema wamechoka kumtafuta ndugu yao, hivyo wanaomba Jeshi la Polisi liwasaidie kumtafuta.

Alisema ndugu wanachotaka kufahamu ni kama mwanamke huyo yupo hai au alishafariki dunia kwa kuwa tangu alipotoweka mwaka 1992, wamekuwa wanaishi katika mazingira magumu.

Naye Mahona Himu, jirani na mama aliyepotea, alisema wana imani kubwa na Jeshi la Polisi kwamba litafanya uchunguzi wa kina kuhusu suala hilo ili ukweli ujulikane na ndugu wawe na amani.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA MARA, SIMIYU NA MANYARA (BABATI DC, HANANG DC, MBULU DC NA BABATI TC)**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na mzunguko wa nne utafanyika katika Mikoa ya Mara, Simiyu, na Manyara katika Halmashauri za Wilaya za Babati, Hanang, Mbulu na Mji wa Babati tarehe 04 hadi 10 Septemba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari litafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 04 hadi Jumanne tarehe 10 Septemba, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 9 na kubonyeza.Kisha atachagua Namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***
**Limetolewa tarehe 27 Agosti, 2024 na:**

Juma Rahisi.
KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana (kushoto), akishukuru na kumpongeza Meneja Maendeleo ya Biashara wa Benki ya NBC tawi la Morogoro, Joseph Boaz (kulia), kwa kutambua mchango wa benki hiyo katika kuchochea maendeleo ya sekta ya utalii nchini, kupitia huduma zake pamoja na udhamini kwenye maadhimisho ya miaka 60 ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Morogoro, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ulimwengu: Ukweli uwekwe wazi kwa maslahi ya nchi

**Na Jenifer Gilla**

MWANDISHI wa habari mkongwe, Jenerali Ulimwengu amewataka waandishi wa habari kuripoti matukio ya nchi kwa njia sahihi, ili ukweli uwekwe wazi kwa maslahi mapana ya nchi.

Amesema waandishi wa habari wengi wameegemea upande mmoja wa kuandika habari chanya, na hiyo inatokana na kutegemea kauli zinazosemwa na wahusika badala ya kufanya uchunguzi.

Ulimwengu alitoa kauli hiyo wakati wa Kongamano la 24 la Jumuiya ya Mawasiliano ya Afrika lililojadili mambo mbalimbali kuhusu tasnia ya habari lililofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), akionya kuwa utegemezi huo "umepoteza waandishi wa habari za uchunguzi".

Alisema hata wale waandishi waliokuwa wakiandika habari za uchunguzi kwa kina, wakifichua mabaya yanayotendeka nchini, wamegeuka kuwa "wasema mazuri na wengine wameajiriwa serikalini".

Alisema si jambo jema kuwa na chombo cha habari kinachosema mambo mazuri tu wakati kuna mambo mabaya yanatendeka, hivyo ni vyema waandishi kujikita kuandika habari za uchunguzi.

"Tusiseme mambo ni mazuri tu wakati kuna mabaya, kama kuna matatizo makubwa lakini kuna jitihada zinaonekana za kushughulikia hayo matatizo basi ziripotiwe hizo jitihada, lakini kama watu wana matatizo na wahusika wamekaa tu hawaoni hayo matatizo, nayo iripotiwe," alisema.

Ulimwengu alisema upungufu huo umesababisha wananchi wengi kukimbilia habari za mitandao ya kijamii kwa kuwa huko hakuna mipaka; matokeo yake wanapata taarifa nyingi za uzushi zinazotolewa na watu ambao hawana taaluma.

"Mimi mwenyewe ambaye chimbuko langu ni kwenye magazeti, sioni haja ya kununua gazeti. Ujue kwamba hali ni mbaya, kwanza ninafikiria nitasoma nini, kumsifu tu mkuu wa mkoa, mkuu wa nchi kafanya hiki, kwamba hiyo ndio kazi ya gazeti? Hapana!" alionya.

Amidi wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Mona Mwakalinga, alisema habari za uchunguzi hazifanywi ipasavyo nchini kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo waandishi kuogopa kuandika taarifa za uchunguzi kwa kuhofia maisha yao.

Alisema uandishi wa uchunguzi ni muhimu kwa sababu ndio unaosaidia jamii kuelewa yanayoendelea katika nchi yao na wale waliopo madarakani kufanya mambo wanayopaswa kwa sababu wakienda kinyume itawekwa hadharani.

Alisema kongamano hilo lililokutanisha nchi 25, lililenga kuwaweka pamoja wataalamu wa sekta hiyo, hasa katoka Bara la Afrika, ili kupitia utafiti wao na kuainisha na kujadili changamoto zinazokabili tasnia hiyo na kuzitafutia ufumbuzi.

"Tunatambua kwamba sauti za Afrika hazisikiki vizuri katika nchi za magharibi, na kama kuna kitu ambacho kinasikika ni zile taarifa ambazo ni mbaya na zina upande mmoja.

"Afrika tuna mchango mkubwa na tuna mambo yetu ambayo tunataka watu wasikie kutoka kwetu, na si kutoka kwa mtu wa tatu au wa nne ambaye hata hajui tupo wapi.

"Waandishi wa habari, huu ndio wakati wa kuonesha jamii kuwa tupo na tunafanya kazi kwa kuwaweka katika nafasi yao wenye mamlaka," alisema.

Mhadhiri na Mkuu wa Idara ya Mawasiliano kwa Umma Chuo Kikuu cha Tumaini, Dk. Samwilu Mwaffisi, alisema waandishi wa habari wanashindwa kuripoti habari za uchunguzi kutokana na kukosa fedha za utekelezaji.

Alitaja sababu ya pili kuwa wengi wanaogopa kujiingiza katika matatizo kupitia mikono ya serikali au, na wale wanaowachunguza.

## Wachumi: Vikwazo vya kibiashara kati ya China, Tanzania vipunguzwe

**Na Frank Monyo**

WATAALAMU wa uchumi wameshauri serikali kupunguza vikwazo vya kibiashara ili kuimarisha biashara kati ya China na Tanzania kwa kuleta uwiano sawa wa kuuza na kuingiza bidhaa kutoka taifa hilo.

Pia wamesema ipo haja wataalamu wa Tanzania kuajiriwa China kama ilivyo kwa Tanzania inavyoajiri watu wa taifa hilo katika baadhi ya kada, kwa kuwa kwa kufanya hivyo kutaongeza ukubwa soko la ajira na biashara kati ya nchi hizo mbili.

Akizungumza na Nipashe jana kuelekea Kongamano la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC) linalotarajiwa kufanyika Beijing kuanzia Septemba 4 hadi 6 mwaka huu, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Dk. Nassib Mramba, alisema mkutano huo unatoa fursa kwa taifa hilo kujadiliana na nchi za Afrika kuhusu misaada, msamaha wa madeni, mikopo ya masharti nafuu na mikopo isiyo na riba.

Rais Samia Suluhu Hassan ameteuliwa kuhutubia wakati wa ufunguzi wa FOCAC, ambako kutakuwa na mkutano wa pembeni baina ya China na Tanzania utakaokwenda sambamba na utiaji saini mkataba wa kulifufua Shirika la Reli la Tanzania na Zambia (TAZARA) lenye miongo mitano.

Alisema China inauza zaidi Tanzania na inaagiza kidogo, akieleza kuwa ni wakati mwafaka kwa kongamano hilo kushughulikia matatizo hayo na kuongeza kuwa ipo haja ya kuangalia suala la fursa sawa za ajira.

"Kilimo kinaajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania, lakini sekta hiyo inachangia asilimia 25 pekee katika uchumi wa nchi. Tunahitaji Wachina kuwekeza katika kilimo cha kisasa, ili kuhakikisha sekta hiyo inachangia zaidi katika uchumi wa nchi," alisema.

Mkurugenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Kichina cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Humphrey Moshi, alisema kongamano hilo ni jukwaa sahihi kwa Tanzania kuimarisha maeneo ya ushirikiano kama vile viwanda, kilimo na biashara.

Prof. Moshi alisisitiza haja ya kuwa na makubaliano ya nchi mbili na kuanza kutumia fedha ya China (Yuan) badala ya kutegemea Dola ya Marekani.

"Pia tunahitaji kutumia jukwaa hili kama fursa kuimarisha uwezo wetu wa mazungumzo na hatimaye kuweka mkakati," alisema.


### KUPOTEA KWA CHETI



**LILIAN FIDELIS GANDYE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA S0268/0024 KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA BETHELSABS GIRLS SECONDARY SCHOOL MWAKA 2012. YEYOTE ATAEFANIKIWA KUKIONA CHETI HICHO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA PHQ/IRI/IRI/13220/2024.

**IN THE RESIDENT MAGISTRAT'S COURT OF MBEYA AT MBEYA**
**CIVIL CASE NO.7584 OF 2024**
**OBO INVESTMENT LIMITED........PLAINTIFF**
**VERSUS**
**OBBY NKONYOTO MDOLLO...DEFFENDANT**
**TO OBBY NKONYOTO MDOLO OF MBOZI**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Judgement on the 05th day of September2024 at 08:30am before Hon P.D. NTUMO-PRM resident Magistrate.
YOU ARE required to appear in this court on the fixed date without fail.
Given under my hand and seal of the Court this 27th day of August2024.

..............................
**RESIDENT MAGISTRATE**

### KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**PETER A. MWANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya TVS KING yenye usajili namba MC 632AAV, CHASSIS NAMBA: MD6M14PK3E4A33282 na ENGINE NAMBA: 0K4AE1046762. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: KAWE POLICE

### KUPOTEA KWA PASSPORT



**PROCHES EDWARD TEMBA** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba TAE 633877 iliyotolewa Makao makuu Dar es salaam PCO mwaka 2023. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/185374/2024**

TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio upangaji matokeo si suala la kusubiri kanuni

**BAADA** ya wadau wengi wa soka kupiga kelele ya kuwa na mdhamini anayedhamini klabu zaidi ya moja kwenye Ligi Kuu, Bodi ya Ligi nchini (TPLB), iliibuka na kusema italifanyia kazi suala hilo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Almasi Kasongo, alisema baada ya kuibuka hoja na mjadala mkubwa kwa wadau wa soka ambao wanadhani kuna haja ya kuzuia mdhamini mmoja kudhamini zaidi ya klabu moja, alisema anakaribisha maoni ya wadau kwa kuwa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), na Bodi ya Ligi wanaendesha soka kwa uwazi na usikivu, hawajafunga milango badala yake wanakaribisha maoni.

Tunapenda tumpongeze Kasongo kwa utendaji wake, kwani mara nyingi amekuwa karibu mno na wadau, akiwasikiliza kile ambacho wanakisema na wakihitaji ufafanuzi.

Hata kwa hili alijitokeza na kulitolea ufafanuzi, ambapo aliwataka wadau wote wanaotaka suala hili libadilike wapeleke maoni yao ili itengenezwe kanuni. Hata hivyo, tayari kanuni za Ligi Kuu msimu huu zimeshatoka na zinatumika, hivyo hizo za kudhibiti wadhamini kama maoni yatapelekwa basi yatasubiri kupitishwa kwa ajili ya msimu ujao wa 2025/26.

Pamoja na hayo, bado tunaona TFF na TPLB wanaweza kufanya lolote sasa hivi juu ya suala hilo kwani hawazuiwi kuamua pale wanapoona kuna viashiria vya kupanga matokeo.

Hatujasema matokeo yamepangwa, bali tumesema viashiria, kwani ukweli uko pale pale kuwa mdhamini yeyote anayedhamini timu zaidi ya moja huku akionekana wazi ana maslahi zaidi na klabu moja zaidi kati ya hizo, ni lazima atafute namna ya kunufaika na upande huo wa pili.

Tujiulize tu kwa mfano rahisi, Kampuni ya Chai, haina timu yoyote ile Ligi Kuu, ikadhamini timu mbili, halafu mwisho wa siku, timu yake moja inahitaji pointi moja tu isishuke daraja na inacheza na timu nyingine ambayo anaidhamini, unafikiri inaweza kushuka? Ni kwamba kampuni itaitaka timu inayoidhamini kuichia na kuipa japo pointi moja isishuke ili iendelee kuitangaza bidhaa yao ya chai kwenye Ligi Kuu.

Ndiyo maana wenzetu Ulaya, hawataki kabisa jambo kama hilo kwa kutengeneza uaminifu ili ligi zao ziaminiwe na zisitiliwe shaka. Inawezekana hakuna chochote kinachoendelea, lakini wadau wengi wanatia shaka kutokana na ukaribu huo wa udhamini. Ndiyo maana hata wanasheria wana msemo wao kuwa pamoja na haki kutendeka, lakini lazima ionekana ikitendeka kweli pasi na shaka.

Mfano ni ule ule wa Arsenal inayodhaniwa na shirika moja la ndege, lakini kwa sheria na kanuni za Ligi ya England hairuhusiwi tena kudhamini timu nyingine katika ligi hiyo, ndiyo maana limekwenda kuidhamini Real Madrid nchini Hispania, AC Milan ya Italia na PSG ya Ufaransa.

Hivyo, TFF na TPLB kusubiri wadau kutoa maoni ni kukwepa majukumu kwani wadau hao hao, wengi wana tabia ya kulalamika tu, hawana utamaduni wa kuandika rasmi maoni yao na kuyawasilisha. Kwa maana hiyo msimu ujao kama wadau hawakupeleka maoni hayo, mdhamini anayelalamikiwa ambaye ni Kampuni ya GSM ataendelea kuzidhamini timu zaidi ya moja kwenye Ligi Kuu?

Lakini pia kwa jicho la karibu tu, hivi TFF na TPLB zinadhani timu ambazo zinadhaminiwa na GSM zinaweza kuunga mkono hoja ya kuondolewa udhamini wao? Ni wazi hawatotoa maoni hayo, pia watakataa kupitisha hoja hiyo.

Kwa maana hiyo jambo hili linaonekana bado lipo mikononi mwao na hawajachelewa kulitokea maamuzi, kwani sisi tukiwa kama wadau namba moja wa soka nchini huku tukiamini katika mchezo wa kiungwana, tunaona ipo haja kwa TFF na TPLB kulifanyia kazi sasa na halihitaji kusubiri maoni ili kuunda kanuni mpya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hatukujiandaa kutumia VAR Ligi Kuu msimu huu

**LIGI** Kuu Tanzania Bara imeanza huku kutumika kwa video ya kumsaidia mwamuzi maarufu kama VAR, ikiwa bado ni kizungumkuti.

Si kwamba hakuna, VAR imeshatua nchini na imefungwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, na ilielezwa kuwa mmoja wa wadhamini wa ligi hii pia angeleta VAR yake inayotembea maarufu kama 'mobile VAR', hii sina uhakika nayo sana kama imekuja au la, lakini ile ambayo iliahidiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), ilizinduliwa Julai mwaka huu.

Awali, kabla ya VAR kutua nchini viongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB), walitanabaisha kuwa msimu huu Ligi Kuu Tanzania Bara baadhi ya mechi zake zitatumia chombo hicho.

Nilimsikia kiongozi mmoja akisema kuwa msimu huu zitatumika VAR mbili, moja ikijikita pale Benjamin Mkapa na nyingine ile ya kutembea 'mobile VAR' itakuwa inakwenda katika mechi za mikoani zenye mvuto na hisia zaidi kwa mashabiki.

**Nilimsikia kiongozi mmoja akisema kuwa msimu huu zitatumika VAR mbili, moja ikijikita pale Benjamin Mkapa na nyingine ile ya kutembea 'mobile VAR' itakuwa inakwenda katika mechi za mikoani zenye mvuto na hisia zaidi kwa mashabiki.**

Ligi Kuu Tanzania Bara ikaanza Agosti 16, mwaka huu, lakini hakukuwa na kitu kama hicho na mashabiki kama kawaida yao wakahoji, kauli ikaja kuwa itatumika baadaye kidogo kwani kwa sasa waamuzi wako kwenye mafunzo.

Ikaeleza kuwa wakufunzi kutoka CAF na FIFA ndiyo wanaosimamia na ikiisha waamuzi watakaofuzu ni lazima kwanza wapasishwe, na pia kipatikane kibali cha kuanza kutumia chombo hicho.

Bado mashabiki wengi waliona inawezekana baada ya raundi tatu za Ligi Kuu, VAR inaweza ikawa tayari. Hii tayari ni raundi ya pili imeingia hakuna mategemeo yoyote ya VAR kuanza kutumika.

Sasa imekuja kugundulika kuwa ili VAR itumike ni lazima wachaguliwe waamuzi kiasi cha 15 hivi waingie kwenye mafunzo angalau ya wiki nne ili kuweza kufuzu kuwa kwenye chumba cha VAR.

Inasemekana mpaka sasa kumbe bado hawajapatikana waamuzi ambao wanatakiwa kuwa kwenye chumba hicho kwa ajili ya kazi hiyo, na sasa kazi ilioanza ni kuanza kuwafundisha.

Siyo jambo baya, lakini cha kujiuliza, wakati mkakati wa kuileta VAR nchini unafanywa, si ilikuwa inafahamika kuwa kunahitajika watu wa kuiendesha? Si ilijulikana kuwa watu hao walipaswa kupata mafunzo kwanza? Au tulidhani mtambo wenyewe wa VAR baada ya kufungwa ndiyo utakuwa 'unajikontroo' wenyewe? Hapana. Tulifahamu kuwa tunahitaji mafundi kwa ajili ya kutengeneza mtambo iwapo utaharibika, pia wataalamu ambao ni waamuzi wanaokuwa wanaendesha kwa engo zote zinazotakiwa pale utata wa matukio utakapojitokeza, na kwa sababu wao pia ni waamuzi wanapoona wanajua ni maamuzi gani yanatakiwa kufanyika.

Haikufanyika hivyo, badala yake mkazo mkubwa ulikuwa kwenye VAR yenyewe na habari kubwa ikawa ni hiyo bila kufahamu watakaoiendesha ni kina nani.

Hiki kilichofanyika ni sawa na mtu kufurahia kununua au kupewa gari, lakini muda wote anafurahia hilo na kupita huku na kule kuwaambia ndugu na rafiki zake, badala ya kuutumia kwenda kujifunza udereva ili likija tu aanze kuendesha.

Badala yake gari limewasili, ndiyo anaanza kujiuliza ataendeshaje, baadaye ndiyo anataka kwenda sasa kwenye mafunzo ya udereva wakati gari limekaa uani.

Angefanya hivyo mwanzo, lingewasili tu na angeanza kuliendesha moja kwa moja, kwani wakati mipango hiyo inafanywa yeye tayari ameshaanza kujifunza.

Wakati mipango ya VAR kuletwa nchini kungekuwa tayari na baadhi ya waamuzi wameshachaguliwa kuanza kujifunza kokote kule, nadhani ligi ilipokuwa inaanza ingewakuta wapo tayari.

Kwa kitendo cha VAR kuja ndiyo mipango ya kufunza watu inaanza, inaonekana kabisa bado hatukuwa tayari kuitumia kwenye ligi yetu msimu huu.

## TANGAZO

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**KIBAHA DISTRICT COUNCIL**

# FINANCIAL STATEMENT FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2023

## STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30TH JUNE, 2023

| | Note | 2023 TZS | 2022 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current Asset** | | | |
| Cash and Cash Equivalents | 62 | 3,907,692,666 | 4,195,493,082 |
| Receivables | 67 | 1,700,152,470 | 472,855,370 |
| Inventories | 70 | 218,383,020 | 71,438,242 |
| Other Financial Assets | 71 | 17,094,000 | 17,094,000 |
| **Total Current Asset** | | **5,843,322,156** | **4,756,880,694** |
| **Non-Current Asset** | | | |
| Property, Plant and Equipment | 77 | 31,714,988,249 | 27,211,368,184 |
| Work In Progress | 82 | 7,408,307,735 | 7,437,557,415 |
| **Total Non-Current Asset** | | **39,123,295,984** | **34,648,925,599** |
| **TOTAL ASSETS** | | **44,966,618,140** | **39,405,806,293** |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current Liabilities** | | | |
| Payables and Accruals | 89 | 2,050,945,144 | 1,756,361,914 |
| Provisions | 92 | 0 | 95,280,000 |
| Deferred Income | 93 | 2,564,393,232 | 1,683,749,481 |
| Deposits | 94 | 1,206,182,369 | 638,144,310 |
| **Total Current Liabilities** | | **5,821,520,745** | **4,173,535,705** |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **5,821,520,745** | **4,173,535,705** |
| **Net Assets** | | **39,145,097,395** | **35,232,270,588** |
| **NET ASSETS/EQUITY** | | | |
| **Capital Contributed by:** | | | |
| Other Reserves | | 17,094,000 | 17,094,000 |
| Taxpayers/Share Capital | | 0 | 0 |
| Accumulated Surpluses / Deficits | | 39,128,003,395 | 35,215,176,588 |
| **TOTAL NET ASSETS/EQUITY** | | **39,145,097,395** | **35,232,270,588** |

................................
**Hon.** Erasto Mpangala Makala
**Council Chairman**
**Date:** 28 March 2024

................................
**Ms.** Regina L. Bieda
**District Executive Director**
**Date:** 28 March 2024

## CASHFLOW STATEMENT AS AT 30th JUNE, 2023

| | Note | 2023 (TZS) | 2022 (TZS) |
|---|---|---|---|
| **CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | | |
| **RECEIPTS** | | | |
| Tax Revenue | 15 | 0 | 0 |
| Subvention from other Government entities | 32 | 24,528,941,721 | 23,264,193,284 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 403,855,198 | 373,591,650 |
| Revenue Grants | 16 | 0 | 0 |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 724,358,326 | 114,722,624 |
| Other Revenue | 31 | 648,348,584 | 3,858,332,379 |
| Levies | 18 | 896,548,323 | 632,546,002 |
| Increase in Deposit | 61 | 568,038,059 | 184,598,784 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 19 | 399,583,500 | 653,555,950 |
| External Assistance | 25 | 2,324,051,929 | 2,205,090,254 |
| 15% Contribution from PSCs | 23 | 0 | 0 |
| **Total Receipts** | | **30,493,725,640** | **31,286,630,927** |
| **PAYMENTS** | | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 34 | 19,497,438,105 | 18,180,994,003 |
| Use of Goods and Service | 35 | 3,666,698,207 | 2,819,325,047 |
| Social Benefits | 43 | 803,211,704 | 1,168,729,223 |
| Other Transfers | 60 | 412,947,915 | 396,681,293 |
| Other Expenses | 52 | 397,077,255 | 719,316,319 |
| Maintenance Expenses | 36 | 796,355,201 | 632,912,133 |
| Grants and Transfers | 59 | 0 | 0 |
| **Total Payments** | | **25,573,728,387** | **23,917,958,018** |
| **NET CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | 4,919,997,254 | 7,368,672,908 |
| **CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | | |
| **Investing Activities** | | | |
| Payment for Work in Progress | 106 | (1,673,116,093) | 2,390,291,415 |
| Advance Payment for Acquisition of Property Plant and Equipment | | 0 | 0 |
| Acquisition of Property, Plant and Equipment | 77 | (3,534,681,577) | (1,681,923,752) |
| **Total Investing Activities** | | **(5,207,797,670)** | **(4,072,215,167)** |
| **NET CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | **(5,207,797,670)** | **(4,072,215,167)** |
| Net Increase | | (287,800,415) | 3,296,457,741 |
| Cash Surrendered to Holding Account | | 0 | 0 |
| Cash and cash equivalent at beginning of period | | 4,195,493,082 | 899,035,341 |
| Cash and cash equivalent at end of period | 62 | 3,907,692,666 | 4,195,493,082 |

................................
**Hon.** Erasto Mpangala Makala
**Council Chairman**
**Date:** 28 March, 2024

................................
**Ms.** Regina L. Bieda
**District Executive Director**
**Date:** 28 March, 2024

## STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE AS AT 30TH JUNE, 2023

| | Note | 2023 (TZS) | 2022 (TZS) |
|---|---|---|---|
| **REVENUE** | | | |
| **Revenue** | | | |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 1,897,594,514 | 215,900,048 |
| Levies | 18 | 885,622,914 | 712,730,411 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 19 | 399,583,500 | 647,725,950 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 403,855,199 | 373,591,650 |
| External Assistance | 25 | 2,324,051,929 | 2,205,090,254 |
| Other Revenue | 31 | 648,348,584 | 3,093,958,276 |
| Subvention from other Government entities | 32 | 23,755,897,286 | 22,520,765,303 |
| **Total Revenue** | | **30,314,953,926** | **29,769,761,892** |
| **TOTAL REVENUE** | | **30,314,953,926** | **29,769,761,892** |
| **EXPENSES AND TRANSFERS** | | | |
| **Expenses** | | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 34 | 19,568,865,013 | 18,291,419,719 |
| Use of Goods and Service | 35 | 3,683,817,058 | 2,775,129,048 |
| Maintenance Expenses | 36 | 796,355,202 | 632,912,133 |
| Depreciation of Property, Plant and Equipment | 37 | 741,751,285 | 774,422,568 |
| Loss on Disposal of Assets | 44 | 20,000,000 | 0 |
| Other Expenses | 52 | 397,077,255 | 719,316,319 |
| Social Benefits | 56 | 803,211,704 | 1,168,729,223 |
| **Total Expenses** | | **26,011,077,517** | **24,361,929,010** |
| **Transfer** | | | |
| Other Transfers | 60 | 486,329,601 | 396,681,293 |
| **Total Transfer** | | **486,329,601** | **396,681,293** |
| **TOTAL EXPENSES AND TRANSFERS** | | **26,497,407,118** | **24,758,610,303** |
| **Surplus / Deficit** | | **3,817,546,807** | **5,011,151,588** |

................................
**Hon.** Erasto Mpangala Makala
**Council Chairman**
**Date:** 28 March, 2024

................................
**Ms.** Regina L. Bieda
**District Executive Director**
**Date:** 28 March, 2024

## REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STSTEMENTS

**1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL**

Hon. Chairperson of the Council,
Kibaha District Council,
P.O. Box 30153,
**KIBAHA.**

**1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS**

**Unqualified Opinion**
I have audited the financial statements of Kibaha District Council, which comprise the statement of financial position as at 30 June 2023, the statement of financial performance, statement of changes in net assets, cash flow statement and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year then ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies.

In my opinion, the accompanying financial statements present fairly in all material respects, the financial position of Kibaha District Council as at 30 June 2023, and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finances Act, Cap. 290.

**Basis for Opinion**
I conducted my audit in accordance with the International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the section below entitled "Responsibilities of the Controller and Auditor General for the Audit of the Financial Statements". I am independent of Kibaha District Council, in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

**1.2.2 Compliance with the Budget Act and other Budget Guidelines**

**Subject matter: Budget formulation and execution**
I performed a compliance audit on budget formulation and execution of Kibaha District Council for the financial year 2022/23 as per the Budget Act and other Budget Guidelines.

**Conclusion**
Based on the audit work performed, I state that, Budget formulation and execution of Kibaha District Council is generally in compliance with the requirements of the Budget Act and other Budget Guidelines.

Charles E. Kichere
**Controller and Auditor General,**
**Dodoma, United Republic of Tanzania.**
**March 2024**

## Madiwani wataka halmashauri kulipa madeni ya watumishi

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

MADIWANI wa Halmashauri ya Chalinze, mkoani Pwani wameitaka halmashauri hiyo kuhakikisha inalipa madeni yote inayodaiwa, yakiwamo ya watumishi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chalinze, Hassan Mwinyikondo, alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki wakati wa Baraza Maalum la kupokea taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha 2023/24, ikibainisha kuwapo deni la Sh. bilioni 3.3.

Alisema ni vema zikatengwa fedha za kulipa madeni hayo ambayo mengine ni ya watumishi ambayo kwa muda mrefu wanayafuatilia na hayajakamilika hadi sasa.

Mwinyikondo alipongeza Halmashauri ya Chalinze kwa kuendelea kuongeza mali za kudumu na kupunguza madeni kila mwaka, jambo ambalo linaifanya kuwa na maendeleo zaidi ambayo yanatatua kero za wananchi wake.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Archanus Kilaja, Ofisa Utumishi, aliahidi madiwani kwamba maelekezo yao yatafanyiwa kazi kwa kuendelea kutenga fedha za kulipa madeni yaliyopo.

Awali akiwasilisha taarifa ya fedha kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24, Mwekahazina wa Halmashauri hiyo, Rehema Lucian alisema madeni yanayodaiwa kwa halmashauri hiyo ni Sh. bilioni 3.3.

Rehema alisema madeni hayo ni ongezeko la asilimia 16.46 kulinganisha na yaliyokuwapo mwaka wa fedha 2022/23 ambayo yalikuwa Sh. bilioni 2.8, yakiwamo ya watumishi Sh. milioni 357.3 na wazabuni Sh. 945,059,252.45.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Juni 30 mwaka huu, halmashauri inaendelea kudai Sh. bilioni 3.2 sawa na punguzo la asilimia 11.26 kulinganisha na madeni ambayo ilikuwa ikidai wateja na wadau mbalimbali katika mwaka wa fedha 2022/23 yenye thamani ya Sh. bilioni 3.6.

Mwekahazina huyo pia alieleza kwamba kwa mwaka wa fedha 2023/2024, halmashauri iliweka makadirio ya makusanyo ya mapato ya ndani Sh. billioni 15.6 na kufanikiwa kukusanya Sh. bilioni 16.2 sawa na asilimia 103 ya makadirio ya bajeti, ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.59 kulinganisha na Sh. bilioni 13.9 za makusanyo ya mapato ya ndani ya mwaka wa fedha 202/23.

# Ridhiwan aonya maofisa kazi kuchafua taswira ya serikali

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI imeelekeza maofisa kazi nchini kutoa taarifa kwa wakati kuhusu wafanyakazi wanaoumia wakiwa kazini, ili wapewe stahiki zao haraka kama sheria inavyoelekeza.

Maofisa hao pia wametakiwa kusimamia maslahi ya wafanyakazi sehemu za kazi kwa uadilifu, weledi na kuondoa malalamiko yasiyokuwa ya msingi dhidi yao.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwan Kikwete, aliagiza hayo juzi jijini Arusha wakati akifungua kikao kazi cha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na maofisa kazi nchini.

Ridhiwan alisema baadhi ya maofisa kazi wa mikoa wamekuwa wakilalamikiwa kwa kushindwa kutatua migogoro na malalamiko ya wafanyakazi, jambo ambalo limekuwa linatoa taswira mbaya dhidi ya serikali.

Alisema serikali imekuwa inajali maslahi ya wafanyakazi, akisisitiza ndicho kiini cha kufanya mabadiliko ya sheria kupitia Muswada wa Sheria ya Huduma za Jamii wa Mwaka 2024.

> **"Ndugu zangu hamkupewa ofisi kuwa vitanda na nyumba zenu za kuishi, ninataka kusikia mnatatua malalamiko ya wafanyakazi na si kuwapatia majibu ya kashfa...**

"Ndugu zangu hamkupewa ofisi kuwa vitanda na nyumba zenu za kuishi, ninataka kusikia mnatatua malalamiko ya wafanyakazi na si kuwapatia majibu ya kashfa kama baadhi yenu ambavyo mmekuwa mnawajibu wafanyakazi," alionya.

Ridhiwan alisema kuwa tangu aingie ofisini amekuwa anapokea malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi kutotendwa haki maeneo ya kazi na kushangaa kwanini yamekuwa yanamfikia yeye ilhali kila mkoa una maofisa kazi.

Mkurugenzi wa Mfuko wa WCF, Dk. John Mduma, alisema mfuko huo umefanya mabadiliko makubwa katika mfumo wa utendaji wake wa kazi, kwamba hivi sasa huduma za mfuko zinapatikana kwa njia ya mtandao.

Kamishna wa Kazi, Suzan Mkangwa, alisema ofisi yake imekuwa inashirikiana na WCF kuhakikisha malalamiko ya wafanyakazi yanatatuliwa kwa wakati.



Spika wa Bunge ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson (kulia), akimpongeza mshindi wa pili wa mashindano ya kupika kwa gesi yaliyoshirikisha mama na babalishe 1,000 jijini Mbeya, Zuwena Kibula. Mashindano hayo yalianza Agosti 27 na kuhitimishwa Agosti 31. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima wa mbaazi walipwa bil. 30/-

**Na Hamisi Nasri,**
NANYUMBU

ZAIDI ya Sh. bilioni 30 zimelipwa kwa wakulima wa Chama Kikuu cha Ushirika Mtwara, Masasi na Nanyumbu (MAMCU), ikiwa ni malipo ya mbaazi kwa msimu huu wa kilimo.

Wakulima wamelipwa fedha hizo baada ya kufanyika minada ya zao hilo inayoendelea mkoani Mtwara.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Makamu Mwenyekiti wa MAMCU alipokuwa akisoma taarifa ya mwenendo wa minada ya mbaazi inayoendelea hivi sasa inayosimamiwa na kuuzwa kwa mfumo wa Soko la Bidhaa (TMX).

Chini ya utaratibu huo, hadi sasa jumla ya minada mitano imefanyika na wakulima wamelipwa minada minne, huku mnada wa tano fedha zake ziko mbioni kulipwa.

Akizungumza mbele ya waandishi wa habari baada ya mnada wa tano kumalizika wilayani Nanyumbu, mkoani Mtwara, Makamu Mwenyekiti wa MAMCU, Bakari Ado alisema zaidi ya Sh. bilioni 30 za malipo ya minada ya mbaazi zimeshalipwa kwa wakulima ambao wameuza zao hilo kwa njia ya mnada pekee.

Alisema kuwa katika minada minne ambayo imefanyika, zaidi ya tani 18,000 zimeuzwa na fedha zake wakulima tayari wameshalipwa.

Alisema bei ya mbaazi ambayo tani hizo zimeuzwa kwa bei ya Sh. 1,850 bei ya juu na bei ya chini ni Sh. 1,600 kwa kilo.

Ado alisema fedha hizo zitanufaisha wakulima katika maisha yao na kujiendesha kiuchumi na familia zao.

Alisema kuwa katika mnada wa tano, MAMCU wameuza zaidi ya tani 2,000 kwa bei ya Sh. 1,750 bei ya juu na chini ni Sh. 1,650 ambapo wakulima wataanza kulipwa fedha zao kuanzia wiki ijayo.

"Tunaishukuru serikali kwa kutusimamia katika mnada wa mbaazi na kupata fedha hizi kupitia zao hili na fedha hizi tunaamini wakulima watafanyia mambo ya msingi," alisema Ado.

Mkulima kutoka Wilaya ya Nanyumbu, Rajabu Bakari, alisema fedha walizopata, zimesaidia kuendesha maisha yao.

Alisema kuwa kwa mnada ya awali bei zilikuwa za juu kati ya Sh. 1,900 hadi 1,800, lakini minada inayoendelea bei zimeanza kushuka siku hadi siku.

Mkulima kutoka wilayani Nanyumbu, Habiba Rashidi alisema kulipwa fedha zao kwa wakati ni jambo jema na la kupongezwa kwa serikali.

Ofisa Usimamizi Fedha Soko la Bidhaa (TMX), Prince Muu, alisema wataendelea kuuza mbaazi kwa njia ya mnada kupitia mfumo huo wa TMX.

Alisema bei ya mbaazi katika soko la dunia awali ilikuwa juu na hivi sasa wakulima wasishangae kuona bei zikiporomoka, hivyo waendelee kupeleka mazao ghalani ili kupata bei zilizopo kwa sasa.



Katibu Tawala Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga, Mwanaid Adadi Rajabu, akizungumza na wananchi, viongozi na wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Kwemkabara juzi, kwenye uzinduzi wa kampeni ya Mtoto wa Leo Samia wa Kesho, yenye lengo la kumaliza changamoto za madawati. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yasimika minara maalumu Ngorongoro

**Na Allan Isack,** NGORONGORO

WATALII wanaokwenda kutalii katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), watanufaika na huduma ya mawasiliano ya mtandao, baada ya serikali kusimika minara maalumu kwa ajili ya kuchochea shughuli za utalii.

Minara hiyo imejengwa na serikali kupitia Mradi wa Tanzania Kidigitali, kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB), lengo likiwa ni kuchochea shughuli za utalii katika eneo hilo la hifadhi.

Mhandisi kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Kelvin Mwakaleke, alisema hayo walipofanya ukaguzi wa minara katika eneo la NCAA.

Alisema awali minara hiyo ilikuwa inatoa huduma ya mawasiliano ya inteneti kwa mfumo wa 2G, lakini kwa sasa imepandishwa hadhi na itatoa huduma ya 4G baada ya serikali kutoa fedha kwa ajili ya kufanyia maboresho.

"Tunaishukuru serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), kwa kushirikiana na WB kwa kutoa fedha kwa ajili ya kusimika na kupandisha hadhi minara hii, hivyo tunatarajia shughuli za utalii zitakwenda vizuri kwa kuwa watalii watakapokuwa kwenye hifadhi yetu wataendelea kupata huduma ya uhakika ya intaneti," alisema.

> **"Tunaishukuru serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), kwa kushirikiana na WB kwa kutoa fedha kwa ajili ya kusimika na kupandisha hadhi minara hii, hivyo tunatarajia shughuli"**

Mratibu wa Mfumo wa Anwani za Makazi, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jamyon Mbungi, alisema katika eneo hilo wanatoa anwani kwenye maeneo yote, ikiwamo ya vitu ambayo ni pamoja na minara ya mawasiliano.

Mkurugenzi wa Uendelezaji wa Mifumo ya TEHAMA kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mohamed Mashaka, alisema kuwekwa kwa huduma hizo ni jitihada zinazofanywa na serikali kuhakikisha huduma za mawasiliano zinawafikia wananchi popote.

Mashaka ambaye ni msimamizi wa Mradi wa Tanzania Kidigitali, alisema katika eneo wamejenga minara ambayo inauwezo mkubwa.

"Kama mnakumbuka Rais Samia ameweka jitihada ya kufungua nchi kupitia Filamu ya The Royal Tour na sisi kama watendaji ni lazima tuhakikishe tunaunga mkono jitihada hizo kwa vitendo na maelekezo yake," alisema. Alisema lengo la kujengwa kwa minara ndani ya hifadhi hiyo, ni kuhakikisha masuala ya utalii yakuwa nchini pamoja na kukuza uchumi wa Tanzania.

Vilevile alisema WB wameridhishwa na kasi ya utoaji wa huduma wa minara hiyo, wameahidi kuendelea kushirikiana na benki hiyo, ili kuhakikisha wanakamilisha ujenzi wa mradi huo kabla ya Uchaguzi Mkuu mwakani.

# OSHA yaeleza umuhimu kulinda uwekezaji rasilimali watu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), umeeleza umuhimu wa kulinda uwekezaji uliofanywa na serikali katika rasilimali watu, kuanzia wanapozaliwa hadi kuajiriwa au kujiajiri katika shughuli za kiuchumi.

Hayo yalisemwa jijini Arusha na Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alipokuwa akiwasilisha mada kuhusu masuala ya usalama na afya kazini kwa viongozi wa matawi ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE).

Alisema hadi kufikia hatua ya mtu kuwa na ujuzi na kuajiriwa au kujiajiri, serikali inakuwa imewekeza kwa kiwango kikubwa ikiwamo kugharamia huduma za afya tangu utotoni.

Hivyo, alitoa wito kwa waajiri na wafanyakazi kuhakikisha katika sehemu za kazi kunakuwa na mifumo madhubuti ya usalama na afya, ikiwamo kuzingatia taratibu zote.

Mwenyekiti wa TUGHE, Joel Kaminyoge, alieleza jinsi wanavyoshirikiana na OSHA katika kutoa elimu ya masuala ya usalama na afya kwa waajiri na wafanyakazi nchini hususani kwa wanachama wao.

Kaminyoge alisema semina hizo zimesaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha maslahi ya wafanyakazi pamoja na kupunguza migogoro mahali pa kazi.

# Nsekela: Haya hapa yameibeba CRDB kuwekeza nje ya Tanzania

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

UBUNIFU na uthubutu umewezesha Benki ya CRDB kuwekeza nje ya nchi, ukiwamo uboreshaji huduma kidigitali sanjari na historia ya Tanzania katika kudumisha amani iliyoko.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye kikao kazi cha wenyeviti wa bodi na watendaji wakuu wa taasisi za umma jijini hapa mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema benki hiyo imefanikiwa kuvuka mipaka kimataifa kwa kuwekeza nje ya nchi kwa kuwa kabla ya kufanya uwekezaji huo, walifanya utafiti wa kutosha ambao uliisaidia benki kufanikiwa na kufikia malengo.

Alisema benki hiyo imeamua kuwekeza nje ya nchi kwa sababu ya uboreshaji utendaji wa kazi, ikiwamo kujiinarisha kimtaji, kutoa huduma pamoja na kujitawanya kimtandao nchini.

Alisema usimamizi bora wa Bodi ya Benki ya CRDB pamoja na uboreshaji huduma za ndani umesukuma benki hiyo kufanya utafiti wa soko na kwenda baadhi ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na wamezipanga kulingana na vipaumbele vyao.

Alisema nchi ya Burundi walikwenda kwa mara ya kwanza kuanza na leo hii wamekuwa watoahuduma bora zaidi.

Alisema katika mkutano huo unaotoa taswira ya uwekezaji na taasisi kujitafakari, si lazima uende nje ya nchi peke yako, bali ni wakati sasa mashirika kukaa kibiashara, hivyo mkutano huo utaleta chachu ya kufikia maendeleo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake wanayataka kupitia uwekezaji.

Aliongeza kuwa katika kuwekeza nje ya nchi, changamoto hazikosekani katika masuala ya lugha, utamaduni , sheria kutofautiana, ikiwamo mtaji ambao lazima uwe mkubwa, hivyo unapotaka kuwekeza lazima ushirikiane na wazawa wa nchi husika.

"Asilimia 90 ya waajiriwa ni wazawa na asilimia 10 iliyobaki ni wataalamu kutoka nchini kwetu na ili ukubalike kuwekeza lazima wazawa wa nchi husika wakubali," alisema.

Nsekela alitaja sababu ya kwenda kuwekeza nje ya mipaka, hasa katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), kwa kuwa wana wateja wengi, pia nchi hizo zimekuwa zinafanya biashara na Tanzania.

"Tunapokwenda kuwekeza kwenye soko la nje ni lazima kufanya utafiti wa kupata taarifa za kule unapotaka kuwekeza, fursa na kuanzia au kununua biashara ambayo utaingia ubia na wadau wa huko.

"Unapokwenda kuwekeza huko, usiende kiujumla, tafuta wadau utakaoingia nao ubia, kuwa na uongozi bora utakaokwenda sambamba na serikali na teknolojia," alisema.

Vilevile, Nsekela alisema uwekezaji waliofanya Burundi ulikuwa rahisi kwa kuwa mtaji wa kuanzisha benki ni mdogo na huko kuna benki 15 tu.

"Wakati tunaingia Burundi mwaka 2021, mtaji ulikuwa Dola za Kimarekani milioni 13 na tuna fanya vizuri katika kapu la nchi hiyo na tumekuwa karibu na jamii na wadau wa maendeleo.

"Tulichojifunza Burundi ukitaka kuwekeza ni lazima uwe na utulivu na kuelewa serikali nini inachotaka na kwenda sambamba nayo," alisema.

Nsekela aliongeza kuwa historia ya Tanzania kutokana na amani iliyopo inawezesha mashirika, taasisi na benki kuwekeza zaidi nje ya nchi na ndio maana CRDB katika nchi za EAC inachanja mbuga katika kiuwekezaji nje ya nchi.





# Wafanyabiashara EAC wapewa tahadhari ugonjwa wa mpox

**Na Samson Chacha,** SIRARI

MKUU wa Wilaya ya Bunda mkoani Mara, Dk. Vicent Naano, amewataka wafanyabiashara wa Afrika Mashariki kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa mpox.

Alitoa tahadhari hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa maonesho ya biashara ya kimataifa 'Cross Border International Expo' yaliyofanyika katika mipaka ya Sirari upande wa Tanzania na Isebania upande wa Kenya.

"Kwa nchi zetu za Afrika Mashariki na washiriki wa maonesho hayo ikiwemo Congo, Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya na Tanzania jitahidini kufanya biashara zenu huku mkichukua tahadhari

**"Kwa nchi zetu za Afrika Mashariki na washiriki wa maonesho hayo ikiwemo Congo, Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya na Tanzania...**

juu ya ugonjwa huu wa Mpox," alisema Dk. Naano.

Kadhalika aliwataka kufuata taratibu za kitabibu ikiwa ni pamoja na kutokusalimiana kwa kupeana mikono, kuepuka kula wanyama wa porini pamoja na kutoa taarifa kwa viongozi na maofisa afya pindi wanapoona mtu mwenye dalili za ugonjwa huo.

Pia aliwataka wafanyabiashara hao kushirikiana kikamilifu kwa kubadilishana uzoevu ili kuleta tija katika nchi zao na kuinuana kiuchumi.

Baadhi ya maofisa biashara akiwamo, Ryoba Thobias kutoka Migori nchini Kenya waliahidi kuimiza wananchi pamoja na wafanyabiashara katika nchi zao ili kuhakikisha wanachukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.



Baadhi ya wanawake kutoka vikundi vya ujasiriamali vya kata za Majohe na Kivule jijini Dar es Salaam, wakiwa katika mafunzo ya kutumia maganda ya matunda kuzalisha wadudu ambao lishe kwa mifugo. Mafunzo hayo yaliandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wazazi wadaiwa 'kukacha' kuwapeleka watoto bweni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZAZI katika Shule ya Sekondari Masengwa wilayani Shinyanga, wamegoma kuwapeleka watoto wao wa kike katika bweni lililojengwa katika shule hiyo, wakidai kushindwa kumudu gharama.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Shule hiyo, Sulu Mlyambele, alisema walifikia hatua ya kuanzisha bweni kwa ajili ya wasichana kutokana na idadi kubwa kupata mimba pamoja na vishawishi vya njiani.

"Lengo la kuanzisha bweni lilikuwa ni kuwalinda watoto wa kike na tatizo la mimba na ndoa za utotoni, lakini cha ajabu wazazi hawaleti watoto wao kuishi hapa," alisema.

Alisema kati ya wasichana 310 ambao wapo shuleni hapo ni 100 tu ndiyo wanaishi bweni.

Alidai gharama za chakula siyo kubwa kama wanavyodai wazazi hao na kuwa wanafunzi walioko bweni wanalipa Sh.100,000 kwa mwaka mzima kwa ajili ya mpishi na kununua mahitaji mengine kikiwamo chakula.

"Wanafunzi wa kutwa wenyenye wanachangia maharage kilo 15, mahindi kilo 15 na kutoa Sh. 500 ambao hupikiwa makande kwa ajili ya kupata chakula wakiwa shuleni kutokana na kuishi umbali zaidi ya km 30," alisema. Baadhi ya wazazi ambao wameshindwa kupeleka watoto wao bweni akiwamo, Grace Mathias, alisema wanashindwa kumudu gharama zake ikiwa ni pamoja na baadhi ya vitu ambavyo vinatakiwa kutolewa shuleni hapo.

Alisema: "Usipokuwa na Sh. 100,000 unatakiwa kutoa mchele, unga wa mahindi kilo 80, maharage kilo 30 na lita moja ya mafuta ya kupikia, hivyo uwezo huo hatuna na kutulazimu tuwanunulie baiskeli kwa ajili ya usafiri".

# Kahama yatekeleza Sera ya Afya kwa vitendo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, amesema serikali wilayani hapa imetekeleza takwa la Sera ya Afya ya Mwaka 2007 kwa kujenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata pamoja na hospitali za wilaya na halmashauri.

Alitoa taarifa hiyo juzi wakati akipokea vifaa tiba vya Sh.milioni 25 vilivyotolewa na Benki ya Exim Tawi la Kahama katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama mkoani hapa.

Alisema serikali imejitahidi kusogeza huduma mbalimbali za kijamii kwa wananchi wanaishi pembezoni hasa huduma za kiafya, lengo likiwa ni kumwondolea adha mgonjwa kutembea umbali mrefu kufuata huduma hizo.

Alisema vifaa vilivyotolewa na benki hiyo vitasaidia kutoa huduma na kuwanufaisha wagonjwa wanaofika hospitali kupata huduma, kuzitaka taasisi nyingine za kifedha kuiga mfano huo ili kuendelea kutatua changamoto katika sekta ya afya nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano cha benki hiyo, Stanley Kafu alisema, utoaji wa vifaa tiba ni mwendelezo wa kuunga mkono juhudi za serikali katika kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya afya nchini.

Alitaja vifaa hivyo kuwa ni pamoja na mashuka 504, mashine 10 za kutolea maji machafu kwa watoto wachanga, mashine za presha 23 pamoja na mashine za oxygen tano, ambavyo vimetolewa kupitia fedha kutoka sehemu ya faida wanayoipata na kurejesha kwenye jamii.

Mganga Mkuu wa Hospitali hiyo, Dk. Baraka Msumi alisema, vifaa hivyo vitasaidia kuwafikia wagonjwa wengi kulinganisha na ilivyo hivi sasa ambapo kwa siku wanahudumia wagonjwa 800 mpaka 1,200.

# Shule ya Msingi Silayo yakumbwa uhaba madarasa

**Na Rose Jacob,** CHATO

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Silayo, Gilbert Kayene, iliyopo wilayani Chato mkoani Geita amesema ongezeko la wanafunzi katika shule hiyo limesababisha kuwapo kwa uhaba wa madarasa.

Hivyo amewaomba wadau mbalimbali kushirikiana kujenga madarasa lengo likiwa ni kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kukabidhiwa vyumba viwili vya madarasa, ofisi ya mwalimu mkuu pamoja na matundu 10 ya vyoo vilivyojengwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), kupitia Shamba la Miti Silayo, kwa Sh.milioni 96.

"Tunapata shida ya mrundikano wa watoto madarasani, ingawa tuliwagawa kwa awamu mbili, asubuhi na mchana lakini hali bado ni mbaya kwa mazingira ya kusomea," alisema Mwalimu Kayene.

Baadhi ya wazazi wa Kijiji cha Mikonto, akiwamo Veronika Yombo waliwaomba wadau kujitokeza kuwasaidia kuwajengea shule au kuongeza madarasa katika eneo hilo ili kuwanusuru watoto na adha ya mrundikano huo ili wapate elimu bora.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Jerome Nestory, alisema huduma ya TFS ya kufadhili miradi ya maendeleo kwa jamii imeleta tija katika kijiji hicho, ambacho kinakabiliwa na tatizo la uhaba wa shule na madarasa huku kikiwa na idadi ya wakazi 8,373 kati ya hao nusu ni watoto.

Mhifadhi Mwandamizi, Juma Mseti, ambaye ni Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Silayo, alisema shamba hilo linazungukwa na vijiji 16 na wananchi wa maeneo hayo wananufaika kwa kupata mafunzo ya utunzaji miti.

Alisema pia ajira za muda 1,000 na zaidi ya wananchi 5,000 wanalima mazao yao ndani ya hifadhi bila gharama yoyote, lengo likiwa ni kuhakikisha jamii inanufaika na kukua kiuchumi.

Nipashe Spoti**ka**



**TIMU NANE ZENYE NAFASI KUBEBA UEFA MSIMU HUU** UK. 12



Federico Chiesa

# ANAPOWEZA KUCHEZEA CHIESA KIKOSI CHA LIVER

**LIVERPOOL, England**

IWAPO ungerejesha muda kabla ya kuanza kwa majira ya joto na hatari ya kubahatisha kwa usajili mkuu ambao Liverpool wangefanya katika ushambuliaji, pengine ungepitia majina machache kabla ya kufika kwa Federico Chiesa.

Juventus walikuwa wakijaribu kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia muda wote wa dirisha dogo na hatimaye Liverpool wakakubali ofa hiyo, na hivyo kuhitimisha dili la thamani ya pauni milioni 11 siku moja kabla ya tarehe ya mwisho.

Akiwa na rekodi mbaya ya majeraha na kushuka kwa kasi kuelekea miaka yake kuu, inaeleweka kwa nini klabu nyingine zilipishana na Chiesa.

Lakini kwa bei ya chini kama hii na kupongezwa kwa muda mrefu kwa mchezaji, ni rahisi vile vile kutambua kwa nini Liverpool walikuwa tayari kuchukua hatua hii.

Uwezo mwingi wa Chiesa na ustadi wa kucheza popote kwenye mstari wa mbele, unaweza kumfanya atumike vizuri na kocha, Arne Slot, katika msimu mrefu na wenye kuchosha.

Hapa tunaangalia ni wapi Liverpool wanaweza kumpanga Chiesa kwenye kikosi chao, twende sasa...

**Upande wa kushoto**

Tatizo la Chiesa katika kucheza kutoka kushoto ni hapa ndipo Liverpool wapo zaidi. Luis Diaz bado hajaacha udhibiti wa eneo hilo tangu kuwasili kwa Slot majira ya joto, licha ya ushindani mkali kutoka kwa Cody Gakpo na Darwin Nunez.

Hata hivyo, mawinga wa pembeni bado wako na hasira, na kama kasi ya Chiesa tayari inapungua, itakuwa rahisi sana kuzoea Ligi Kuu kuingia ndani badala ya kuelekea kwenye mstari wa mbele.

Juventus walikuwa na tabia ya kucheza bila mawinga wakati Chiesa alipokuwa klabuni hapo, badala yake walitumia mfumo mwaminifu wa Max Allegri wa 3-5-2. Wakati huo, Chiesa mara nyingi alikuwa akicheza nyuma ya mshambuliaji mwenye nguvu zaidi.

Sasa, Liverpool hawana fowadi mwenye nguvu au mnyama kama Dusan Vlahovic, lakini wana wachezaji kama Gakpo na Nunez waliotajwa hapo juu ambao wanaweza kutimiza jukumu kama hilo.

Shida itakuwa kuwaweka kwenye mfumo ambao hausumbui washambuliaji wao wengine. Bado, ni vizuri kuwa na chaguo, na mtaalamu mahiri kama Slot atafurahi kujaribu kupata matumizi kwa pande zote.

**Mshambuliaji pekee**

Jukumu kuu la wazi zaidi katika mfumo chaguo-msingi wa Liverpool litakuwa kama namba tisa.

Tena, Gakpo na Nunez wana uwezo wa kucheza huko pia, lakini kwa kweli amekuwa Diogo Jota ambaye amevutia mapema katika umiliki wa Slot.

Iwapo Chiesa bado atakuwa na ugumu wa kuzoea, labda yeye pia anaweza kuanza kama mshambuliaji.

**Upande wa kulia**

Je, tunatarajia Mohamed Salah atapoteza nafasi yake katika mlengo wa kulia hivi karibuni? Hapana. Na je, tunategemea Federico Chiesa ataweka pambano kuanzia winga ya kulia? Pia hapana.

Lakini Liverpool sasa wana aina mbili za kina kusaidia kusimamia dakika za mfalme wao wa Misri, huku Harvey Elliott akichukua nafasi ya mchezaji wa kushoto na Chiesa chaguo la winga wa asili.

## ISIKUPITE

HAT-TRICK aliyofunga Erling Haaland Jumamosi wakati Manchester City ikishinda 3-1 dhidi ya West Ham United, inamfanya kufikisha mabao 70 katika michezo 69 ndani ya miamba hiyo na pia ilikuwa hat-trick yake ya 11 kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England. Pia hilo ni bao lake la saba katika mechi tatu za Manchester City hadi sasa - ikiwa ni mabao manne zaidi ya mchezaji mwingine yeyote msimu huu kwenye ligi hiyo.



## Extra Time

# TIMU NANE ZENYE NAFASI KUBEBA UEFA MSIMU HUU



Real Madrid

**MONACO, Ufaransa**

LIGI ya Mabingwa Ulaya iliyopanuliwa na yenye sura mpya ipo tayari kutoa hadithi za kufurahisha zaidi msimu huu wa 2024/25.

Real Madrid waliongeza pengo kati yao na timu nyingine mwishoni mwa msimu uliopita na kutwaa Kombe la 15 la Ulaya baada ya kuifunga Borussia Dortmund kwenye fainali. Lazima utupe jicho lako hadi AC Milan kwa klabu iliyo na ushindi mkubwa zaidi katika nafasi ya pili kwenye mashindano hayo, kwani miamba hao wa Italia wakijivunia mataji saba.

Lakini, Ligi ya Mabingwa ya msimu huu itakuwa kubwa kuliko hapo awali. Timu nne zaidi zitashiriki katika kinyang'anyiro hicho, huku hatua ya makundi ikiwa imefutwa na sasa itachezwa kwa mfumo wa ligi.

Kwa kuzingatia hilo, hizi ni timu nane zinazopewa nafasi kubwa zaidi ya kubeba taji hilo msimu wa 2024/25.

### 8. Inter Milan

Inter ilitwaa taji la Serie A msimu uliopita baada ya kukaribia sana ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2022/23. Kupoteza mchezo wa mwisho kwa bao 1-0 dhidi ya Manchester City katika mechi ambayo ingeweza kwenda kwa namna yoyote ile, ilihisi kama nafasi iliyokosa kwa klabu hiyo ya Milan.

Rekodi yao ya Ulaya imekuwa mbaya sana tangu ushindi wao wa mwisho mnamo 2010 na walitoka kwenye 16-bora kwa mara nyingine tena muhula uliopita. Lakini Simone Inzaghi ameifanya 'Nerazzurri' hao kuwa moja ya timu ya kuvutia zaidi barani Ulaya na Lautaro Martinez ambaye yuko katika kiwango chake bora ataingia 2024/25 akiwa mpya baada ya kuiongoza Argentina kubeba Ubingwa wa Copa America.

Si zaidi ya uwezekano kwamba Inter wanapigania taji kufikia hatua za mwisho za msimu, lakini kuna timu kadhaa ambazo zinachukuliwa kuwa bora zaidi.

### 7. Paris Saint-Germain

Paris Saint-Germain wamepata baadhi ya njia za ajabu za kupenya katika hatua za mwisho za Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kwa wamiliki wa klabu wa Qatari, ni tuzo kuu, na ambayo bado haipatikani.

Msimu wa 2023/24 ulikuwa mwito mwingine wa karibu kwa mabingwa wa Ligue 1, ambao walifika nusu fainali chini ya Luis Enrique. Baada ya biashara nzuri ya uhamisho wa majira ya kiangazi mwaka jana na Kylian Mbappe akiwa katika hali ya kuondoka, ilikuwa ni moja ya kampeni zao za kuvutia Ulaya kwa miaka ya hivi karibuni.

Lakini sasa wanatakiwa kuwapiku Real Madrid na historia inaonesha kwamba inaweza kuwa ngumu sana kwa PSG kutwaa Kombe la kwanza la Ulaya.

### 6. Barcelona

Kipigo kibaya cha Barcelona katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya PSG msimu uliopita, kilikuwa moja ya sababu kuu za kutimuliwa kwa Xavi. Kwa kocha mpya Hansi Flick, wana mtu mwenye uzoefu wa kunyanyua kombe la Ligi ya Mabingwa.

Mjerumani huyo alishinda shindano na Bayern Munich msimu wa 2019/20 na atakuwa na nia ya kuongeza kombe la pili la Ulaya kwenye orodha yake ya heshima huko Katalunya. Matatizo yanaendelea ndani na nje ya uwanja kwa 'La Blaugrana' hao, lakini bado wana kikosi chenye vipaji vya hali ya juu.

Itakuwa changamoto kwa Flick kurudia ushujaa wake wa Bayern katika msimu huu wa 2024/25 na Barca bado wanajikuta katika vivuli vya wapinzani wa Clasico, Real Madrid linapokuja suala la mafanikio ya Ulaya.

### 5. Bayern Munich

Bayern pia walitinga hatua ya nusu fainali msimu wa 2023/24, chini ya Thomas Tuchel, lakini wakashindwa na mabingwa Real Madrid na kuwanyima fainali kwa mara ya pili katika karne ya 21 kwenye Uwanja wa Wembley.

Kumwajiri Vincent Kompany kama mbadala wa Tuchel kwa hakika kuliibua hisia. Mbelgiji huyo alishushwa daraja na Burnley msimu uliopita na hana uzoefu wa kusimamia katika kiwango cha juu kama hicho.

Hata hivyo, beki huyo wa zamani wa Man City ana falsafa ya kipekee inayozingatia soka la hatari, la pasi za juu, jambo ambalo linaweza kufaa kwa kikosi cha Bayern.

Kwa hakika mambo hayawezi kuwa mabaya zaidi kwa 'Bavaria' mnamo 2024/25 baada ya msimu usio na taji chini ya Tuchel.

### 4. Liverpool

Sawa na Barcelona na Bayern, Liverpool wanajikuta chini ya usimamizi mpya msimu huu wa 2024/25. Kuondoka kwa Jurgen Klopp mwishoni mwa msimu uliopita kumeacha pengo kubwa, ambalo kocha wa zamani wa Feyenoord, Arne Slot, amepewa jukumu la kuliziba. Dalili za mwanzo ni chanya.

Mashabiki wa Liverpool hawatarajii taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya katika msimu ambao umehakikishiwa kuwa wa mpito, lakini historia ya 'Wekundu' hao kwenye kinyang'anyiro hicho inamaanisha hawawezi kufutwa kamwe. Wakiwa na mastaa kama Mohamed Salah, Trent Alexander-Arnold na Alexis Mac Allister katika safu yao, wako katika nafasi nzuri ya kunyakua kombe lao la saba la Ulaya.

Bila shaka, inabaki kuonekana jinsi mabadiliko ya mbinu yanayofanyika chini ya Slot yatakavyofanya kazi katika Ligi ya Mabingwa, lakini baadhi ya bunduki nyingine kubwa za Ulaya pia hujikuta katika nyakati za kutokuwa na uhakika. Je, Liverpool inaweza kuchukua faida?

### 3. Arsenal

Mashindano ambayo Arsenal wangependa kushinda kuliko mengine yoyote. 'Washikabunduki' walirejea kwa nguvu kwenye shindano hilo msimu wa 2023/24 baada ya miaka mingi kupita, na kufika robo fainali kwa fujo. Lakini kwenye hatua kubwa, waliganda.

Arsenal walipewa nafasi kubwa ya kucheza mechi ya nane bora dhidi ya Bayern, lakini walishindwa kutokana na matarajio yao. Mikel Arteta atakuwa na matumaini kwamba uzoefu kama huo utakuwa wa manufaa kwa miamba hao wa Kaskazini mwa London kwa kampeni ijayo ya Ligi ya Mabingwa.

Arsenal wameonesha dalili chache za kupunguza kasi ya kutafuta umaarufu wa ndani na Ulaya na wana kikosi kinachofikia ubora wake, huku kukiwa na wachezaji wengi wa kubadilisha mchezo ndani ya safu zao.

### 2. Manchester City

Man City walikuwa wanapewa nafasi kubwa ya kutetea taji lao la Ligi ya Mabingwa msimu wa 2023/24 na kama haikuwa kwa mikwaju kadhaa ya penalti walizokosa kwenye mechi ya robo fainali dhidi ya Real Madrid, wangefanya vema.

Mabingwa wa 2022/23 wanaonekana kuwa na uwezekano wa kujituma katika shindano la msimu huu na hakuna chochote kinachowazuia kutwaa ushindi wa pili.

Wana kipa wa kiwango cha dunia, safu ya mabeki wa hali ya juu, kiungo bora zaidi wa ulinzi duniani, mastaa wabunifu wa ajabu na mmaliziaji asiyechoka anayeongoza safu hiyo.

### 1. Real Madrid

Mabingwa watetezi Real Madrid wamepata haki ya kuchukuliwa kupendekezwa kwa msimu wa 2024/25. Ukweli kwamba wamemwongeza Mbappe kwenye kikosi chao chenye nyota wengi, huongeza tu nafasi yao ya kutwaa Kombe la 16 la Ulaya.

Vijana wa Carlo Ancelotti tayari wana taji la Ulaya mfukoni mwao baada ya kushinda UEFA Super Cup katikati ya Agosti na wana uwezekano wa kuimarika kadri msimu unavyoendelea. Mchezaji nyota wao Mfaransa anapozoea mazingira mapya, inatisha kufikiria ubora wanaojivunia uwanjani na dimbani.

Utakuwa jasiri kuweka dau dhidi ya Real Madrid katika kampeni yoyote ya Ligi ya Mabingwa. Uhusiano wao na ushindani ni wa ajabu na uwezo wao wa kuendeleza vipigo na bado kuibuka kidedea ni wa pili.

## Nukuu

"Sijui kama nitamaliza hivi karibuni au baada ya miaka miwili au mitatu. Lakini, ikiwezekana, itakuwa pale Al Nassr. Ni timu ambayo nina furaha, niko vizuri, ninapojisikia vizuri, kote nchini na kwenye ligi. Ndio maana, kuna uwezekano mkubwa naweza kumalizia soka langu Al Nassr. Nina furaha sana kucheza ligi ya Uarabuni na ninataka kuendelea," **Mshambuliaji wa Al Nassr na Ureno, Cristiano Ronaldo.**



"Amefunga mabao matatu leo [juzi], lakini hakupoteza mpira hata mmoja ni kati ya michezo ambayo amecheza vizuri katika hali zote. Unapoona michezo na kuona tunachotaka kufanya, anaelewa kwa sababu ni mtu mwenye akili. Nguvu zake, lugha yake ya mwili imekuwa bora," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, baada ya Erling Haaland kufunga hat-trick ya pili mfululizo wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya West Ham United juzi.**



"Mfano wangu wa kuigwa walikuwa Didier Drogba na Frank Lampard na sasa nina fursa ya kuchezea klabu hii kama wao. Ni hisia nzuri. Nataka kuleta msisimko," **Jadon Sancho baada ya kujiunga rasmi na Chelsea akitokea Manchester United.**





Beki wa kati wa Simba, Che Fondoh Malone, akifunga bao kwa kichwa kwenye Ligi Kuu dhidi ya Tabora United hivi karibuni.

# SIMBA WAIKAMATA LIGI KUU MABAO YA VICHWA

**Na Adam Fungamwangwo**

JUMLA ya mabao 22 yamefungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Mabao hayo yamepatikana kwa michezo 13 iliyochezwa kwenye ligi ambayo kwa sasa imesimama kupisha michezo ya kimataifa kwa timu za taifa ambazo kuanzia keshokutwa zitakuwa mzigoni kwa ajili ya kusaka tiketi za kucheza fainali za Mataifa Afrika zitakazochezwa mwakani nchini Morocco.

Mabao hayo yamefungwa na wachezaji 21, lakini ni matano tu yamefungwa kwa vichwa.

Takwimu zinaonesha kuwa mpaka sasa ni timu mbili tu kwenye Ligi Kuu zilizofunga mabao kwa njia hiyo, nazo ni Simba na Singida Black Stars tu.

Simba ndiyo inayoongoza kwa wachezaji wake kutupia kwa vichwa, ikiwa imefanya hivyo mara tatu na Singida Black Stars mara mbili.

Katika makala haya tunakuletea majina ya wachezaji waliofunga mabao ya vichwa mpaka sasa, mechi walizofanya hivyo na jinsi walivyoyapachika...

**1# Che Fondoh Malone (Simba vs Tabora United)**

Beki huyu wa kati ndiyo mfungaji wa bao la kwanza kwa Simba msimu huu. Alilifunga kwa kichwa Agosti 17 katika mchezo ambao ilicheza dhidi ya Tabora United, Uwanja wa KMC uliopo Mwenge, Dar es Salaam, ikishinda mabao 3-0.

Ilikuwa ni dakika ya 13, ambapo Che Fondoh Malone, raia wa Cameroon, aliporuka juu na kuunganisha kwa kichwa krosi ya Jean Charles Ahoua, ambaye alipasiwa kona fupi na Joshua Mutale.

**2# Elvis Rupia (Singida Black Stars vs KenGold)**

Straika Elvis Rupia, raia wa Kenya, naye yupo kwenye orodha ya wachezaji waliofunga mabao ya vichwa mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alifunga bao hilo, Agosti 17, mwaka huu, wakati timu yake ya Singida Black Stars ilipocheza dhidi ya KenGold, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na kuiongoza timu yake kushinda mabao 3-1.

Akiwa katikati ya mabeki wa KenGold, aliruka juu na kuunganisha mpira wa krosi iliyotoka winga ya kulia kwa Ande Koffi, akaujaza wavuni na kuwa bao la pili katika mchezo huo.

**3# Valentino Mashaka (Simba vs Tabora United)**

Straika huyu Mtanzania aliyesajiliwa na Simba kutokea Geita Gold, ameingia kwenye rekodi ya wachezaji waliopachika mabao ya vichwa mpaka sasa, akiwa amefanya hivyo, Agosti 17, mwaka huu, katika mchezo ambao timu yake ilicheza dhidi ya Tabora United, Uwanja wa KMC, Dar es Salaam, ikishinda mabao 3-0.

Ilikuwa ni dakika ya 67, ambapo Mohamed Hussein 'Tshabalala' alipokokota mpira kwenye wingi ya ksuhoto na kupiga krosi iliyowapita mabeki wa Tabora United vichwani, mwishoni ulimkuta Velentino Mashaka aliyekuwa ameruka juu na kuupigwa kichwa cha kumpoteza kipa mwelekeo, mpira ukatulia ndani ya vyavu, ikiwa ni bao la pili katika mchezo huo.

**4# Mohamed Domaro (Singida Black Stars vs KenGold)**

Mohamed Damaro ni kiungo mpya wa Singida Black Stars, raia wa Guinea naye alifunga bao kwa kichwa katika mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya KenGold, Agosti 17, mwaka huu, na kushinda 3-1, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Alifanya hivyo dakika tisa kabla ya mechi hiyo ya Ligi Kuu kumalizika, akiunganisha kona iliyochongwa na kiungo mwenzake raia wa Togo, Marouf Tchakei, na likawa bao la tatu katika mchezo huo.

**5# Edwin Balua (Simba vs Fountain Gate)**

Winga wa Simba, Edwin Balua, aliukwamisha mpira kwa kichwa Agosti 25, mwaka huu, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, wakati timu hiyo ilipokipiga dhidi ya Fountain Gate na kuondoka na ushindi wa mabao 4-0.

Aliunganisha dakika ya 13 krosi fupi kutoka kwa kiungo mshambuliaji raia wa Ivory Coast, Jean Charles Ahoua kutoka wingi ya kulia.

Baada ya bao hilo ni kama alikuwa amefungulia mabao kwa wenzake, ingawa walifunga kwa miguu.

## JE, WAJUA?



KWA mujibu wa mtaalamu wa masuala ya uhamisho wa wachezaji, Ben Jacobs, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 29, alilazimika kukubali kupunguza mshahara wake wa pauni 325,000 kwa wiki alikuwa akipokea Chelsea, kwa asilimia 50 ili kufanikisha dili lake la kujiunga na Arsenal, na klabu hiyo ya Kaskazini mwa London, 'The Gunners' hatalipa ada ya mkopo.



# Wazazi wapewa mbinu kudhibiti ulawiti kwa watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na ongezeko la matukio ya ulawiti na matukio ya ukatili kwa watoto wa kiume, wazazi wameshauriwa kuweka utaratibu wa kuzungumza na watoto wao wakati wote, ili kujua changamoto wanazopitia wakiwa shuleni na nyumbani.

Wito huo umetolewa juzi jijini Dodoma na Kaimu Ofisa Elimu Mkoa wa Dodoma, Prisca Myala, alipokuwa akizungumza kwenye mahafali ya pili ya darasa la saba ya Shule ya Msingi na Awali ya East Africa Dodoma.

Myala alisema kutokana na ongezeko kubwa la matukio ya ubakaji na ulawiti kwa watoto wa kiume wazazi wanapaswa kuongeza ukaribu na watoto wao, ili kujua madhira wanayopitia wakiwa shule, njiani na hata nyumbani.

"Wazazi lazima muweke utaratibu wa kuzungumza na watoto. Wakati mwingine watoto wanataka kutushirikisha changamoto zao lakini hatuwapi nafasi ya kujua nini wanakabiliana nacho wakiwa shuleni, njiani ama nyumbani," alisema.

Alisema wazazi wengi wamekuwa hawana muda wa kuzungumza na watoto wao kutokana na kutumia muda mwingi kwenye utafutaji wa riziki.

**"Kinamama tusisahau jukumu letu la asili la malezi kwa watoto wetu kinababa wako bize na utafutaji wa maisha hata kama ni hamsini kwa hamsini. Lakini hatupaswi kusahau jukumu...**

"Kinamama tusisahau jukumu letu la asili la malezi kwa watoto wetu kinababa wako bize na utafutaji wa maisha hata kama ni hamsini kwa hamsini. Lakini hatupaswi kusahau jukumu letu la asili la kulea watoto na kuwapa ulinzi," alisema.

Aidha, alisema kutokana na mmomonyoko wa maadili hivi sasa katika jamii hakuna mtu wa kumwamini kwa watoto hata kama ni ndugu wa karibu.

Alisema: "Hata ndugu siyo watu wa kuwaamini kabisa. Kuna ndugu wa karibu ambao wanawalawiti watoto, hivyo hakuna mtu wa kumwamini kwa mtoto wako kama unataka mtoto wako awe vile unavyotaka hauna budi kumlinda kwa sababu dunia ya sasa siyo kama ile ya zamani mambo yamebadilika sana."

Mkurugenzi wa Shule ya Msingi na Awali East Africa, Dk. Rose Rwakatare, alisema lengo lao ni kufanya uwekezaji katika sekta ya elimu, ili kuunga mkono jitihada za serikali kuboresha elimu na kuongeza ufaulu kwa mkoa huo.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kuanzisha mitaala mipya ambayo itakwenda kusaidia watoto wetu kujifunza kwa vitendo na sisi tunaendelea kuwekeza katika sekta ya elimu ili kuupandisha chati mkoa huu kielimu," alisema Dk.Rose

Hata hivyo, aliwataka wazazi ambao wamekuwa na tabia ya kushawishi watoto wa kike kufanya vibaya kwenye mitihani ya darasa la saba ili waolewe kuacha tabia hiyo, kwa kuwa huo ni ukatili.

Alisema: "Mimi nikiwa kama mdau wa elimu nchini suala hili la wazazi kuozesha watoto waliomaliza darasa la saba ni kuwanyima haki yao ya msingi na ni kosa kisheria, hivyo wawaache watoto hawa wapate haki yao ya msingi".

## Udumavu kwa watoto Dodoma wapungua

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UTAFITI wa Kidemografia na Masuala ya Afya wa Mwaka 2022 umeonesha kwamba utekelezaji wa afua za lishe kwa Mkoa wa Dodoma umeendelea kukabiliana na hali ya udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka asilimia 37 hadi kufikia asilimia 30.

Akizungumza mwishoni mwa wiki jijini hapa kwenye kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa Julai-2023 hadi Juni 2024, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema hali ya udumavu imepungua kutokana na kuimarishwa masuala ya lishe.

"Pamoja na kupungua hali bado siyo nzuri kwa kuwa kati ya watoto wenye umri huo 100, wenye udumavu ni 30, ingawa hali ya utekelezaji wa afua za lishe kwa mkataba huu inaendelea kuimarika," alisema.

Hivyo, alitoa tahadhari dhidi ya ugonjwa wa mpox ambao umeathiri watu kadhaa kutoka mataifa jirani.

"Serikali kupitia Wizara ya Afya imetoa taarifa ya kuwapo kwa mlipuko wa ugonjwa wa mpox katika nchi zinazotuzunguka, ugonjwa huu unasababishwa na virusi, tunamshukuru Mungu nchi yetu ipo salama na hakuna taarifa ya uwepo wa mgonjwa," alisema.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Kaspar Mmuya, alisisitiza suala la upandaji miti ya matunda kwa wanafunzi kwa kipindi cha miaka wanayokaa shuleni ili kuimarisha lishe kwa kupata uhakika wa matunda ya kutosha.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akizungumza jijini Mwanza mwishoni mwa wiki katika ziara yake ya kuhamasisha vita dhidi ya ukatili wa kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Madiwani wataka wenyeviti vijiji, vitongoji kulipwa posho

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida wameitaka serikali kuangalia uwezekano wa kuanza kuwalipa kiinua mgongo wenyeviti wa vitongoji na vijiji, wanapomaliza kutumikia nafasi zao kama ilivyo kwa madiwani na wabunge.

Wakizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha baraza la madiwani la halmashauri hiyo, walisema viongozi wa serikali za mitaa wamekuwa wakifanya kazi nzuri ikiwamo kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo kwa ufanisi, hivyo kuna umuhimu na wao waanze kulipwa kiinua mgongo.

Diwani wa Kata ya Tumuli, Bilali Msengi alisema: "Viongozi wa vijiji na vitongoji wamefanya kazi nzuri sana ndani ya miaka mitano kwa kusimamia miradi ya maendeleo, wamesimamia utawala bora na wametoa huduma ndani ya saa 24 katika maeneo yao ya kiutalawa, hivyo serikali ije na wazo la kuanza kuwapa mafao". Msengi alisema mbali na kuwalipa mafao lakini viongozi hao wawe wanajengewa uwezo kwa kuwapa mafunzo na kuwajengea ofisi, ili wawe wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi kwani ni viongozi ambao wapo karibu zaidi na wananchi katika maeneo yao ya kiutawala.

Katika hatua nyingine, Diwani wa Kata ya Mwanzega, Bosco Samweli, alisema jamii ya Wahadzabe ambao wanaishi katika Kijiji cha Munguli Wilaya ya Mkalama wameanza kuondoka na kuhamia katika Mkoa wa Manyara kufuatia maeneo yao waliokuwa wakiishi kuvamiwa na watu kwa kukata miti ovyo.

Alisema jamii hiyo wamekuwa wakiishi msituni katika kijiji hicho na kuendesha shughuli zao zikiwamo kulina asali na kuwinda wanyama, lakini kutokana na uvamizi wa watu kumewalazimu waondoke.

Samweli aliiomba serikaii kuchukua hatua kwa watu waliovamia maeneo wanakoishi jamii ya Wahadzabe ili wasiendelee kuhama makazi yao kwa sababu ni jamii muhimu katika masuala ya utalii.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Mohamed Atiki, akijibu maswali ya madiwani hao alisema ni kweli viongozi wa vijiji na vitongoji wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya kusimamia miradi ya maendeleo kutokana na serikali kutoa fedha nyingi za kutekeleza miradi.

Alisema halmashauri itaandaa utaratibu mzuri kwa kuwapa motisha kutokana na juhudi wanazofanya na pindi mambo yakiwa mazuri suala la uwezeshwaji litafanyika.



Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, akibebwa na kinamama wa Jimbo la Tukuyu waliofika katika warsha ya kuwapa elimu na kuwagawia majiko ya gesi ya Oryx na kuwapatia vitenge zaidi ya wanawake 500 waliojitokeza kutoka vyama vya CHADEMA na CCM, iliyofanyika mwishoni mwa wiki katika Kata ya Kimo wilayani Rungwe. **PICHA: MPIGAPICGA WETU**

# Dk. Tulia: Tumuunge mkono Samia matumizi nishati safi

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson amesema kuna kila sababu ya kuendelea kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan ambaye Afrika inamtambua kama kinara wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Alisema hayo juzi jijini Mbeya wakati akitoa shukrani kwa wadau walioshiriki kufanikisha mashindano ya kupika kwa gesi ya oryx yaliyoshirikisha baba na mama lishe 1,000 kutoka kata za Jiji la Mbeya.

"Tumefanya mashindano haya ya kupika kwa gesi kwa baba na mama lishe kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan ambaye kama mnavyofahamu yeye ndiye kinara wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia Afrika," alisema Dk. Tulia.

Dk. Tulia ambaye ni Spika wa Bunge alisema matumizi ya nishati safi ya kupikia inasaidia kulinda mazingira, kwamba majiko na mitungi ya gesi ya oryx waliyopewa kundi hilo ikawe chachu kutoka hatua moja kwenda nyingine.

Aidha, aliwashukuru oryx ambao wamekuwa wakiungana naye katika matukio mbalimbali yanayohusu wananchi na hasa kwa kuendelea kuwezesha jamii kupata mitungi na majiko. Dk. Tulia alisema: "Tunawashukuru kwasababu mbali ya kutoa majiko 1,000 kwa baba na mama lishe wote walioshiriki mashindano haya pia mmetoa na mitungi mikubwa na majiko yenye sahani mbili kama zawadi kwa washindi, hivyo wanakwenda kukuza biashara zao."

> **Dk. Tulia alisema: "Tunawashukuru kwasababu mbali ya kutoa majiko 1,000 kwa baba na mama lishe wote walioshiriki mashindano haya pia mmetoa na mitungi mikubwa na majiko ...**

Naye Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, aliyekuwa mgeni rasmi wakati wa kuhitimishwa mafunzo hayo yaliyoanza Agosti 27 hadi 31 alisema kumekuwa na jitihada mbalimbali za serikali za kuhakikisha wananchi wanatumia nishati safi ya kupikia.

Judith alisema kukiwa na uwezekano wa gesi kununuliwa kidogo kidogo kutawasaidia wananchi wengi kutumia gesi na hivyo kusaidia kupunguza uharibifu wa mazingira.

Kuhusu tamasha hilo la mapishi, Naibu Waziri huyo alimpongeza Dk. Tulia kwa kuandaa kwa sababu yamekuwa ya mfano na yametumika kutoa elimu ya nishati na utunzaji mazingira.

Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman, alisema lengo kuu la mashindano ya mapishi ni kuhamasika matumizi ya nishati safi kwa lengo la kulinda mazingira.

Alisema: "Kwa miaka zaidi ya 15 iliyopita upatikanaji wa nishati ya kupikia umekuwa ukipangwa na kujadiliwa lakini hivi sasa serikali imekuwa na hamasa kubwa ya kuhimiza wananchi kutumia nishati safi ya kupikia".

Akizungumza kwa niaba ya machifu wa Mkoa wa Mbeya, Chifu Rocket Mwashinga, aliwaomba viongozi wa serikali na wadau wa gesi kuangalia uwezekano wa kupunguza bei ya gesi, ili wananchi waweze kumudu gharama.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho Taifa (NEC), Ndele Mwaselala alimpongeza Dk. Tulia na taasisi yake kwa kuanzisha tamasha hilo, akisema kuwa ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya chama hicho.

## Viongozi wa dini wapewa jukumu kukemea utekaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa dini nchini wametakiwa kukemea vitendo vya utekaji wa watu na mauaji yanayoendelea katika maeneo mbalimbali nchini, wakidai kuwa vitendo hivyo vinakiuka haki za binadamu na ni kinyume na matakwa ya dini.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Imamu wa Msikiti wa Isanga jijini Mbeya, Sheikh Ibrahim Bombo, alisema vitendo hivyo vimekuwa vikisikika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa wakitekwa na kupotea bila sababu, huku baadhi wakiuana kwa sababu ya wivu wa mapenzi, kugombea mali za urithi na nafasi za uongozi.

Alisema endapo viongozi wa dini wataungana kukemea vitendo hivyo na serikali ikatimiza wajibu wake, mauaji na vitendo vingine viovu vitapungua na hivyo kuifanya Tanzania iendelee kuwa mahali salama pa watu kuishi.

Hivyo, aliwataka Watanzania kuondoa chuki baina yao na kuhakikisha wanapatana kwenye masuala yote wanayoingia kwenye migogoro, ili kuepusha vitendo vya mauaji na kutekana ambavyo alisema vinalichafua taifa.

Alisema hakuna dini yoyote duniani ambayo inaruhusu mtu mmoja kumuua mwenzake kwa namna yoyote na hivyo akasisitiza kwamba vitendo hivyo vya mauaji ni haramu.

# RC akerwa tabia w'biashara kuwakimbia maofisa TRA

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amewaonya wafanyabiashara mkoani hapa kuacha tabia ya kufunga maduka na kuwakimbia watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ambao wanafika kwenye maeneo yao kufanya ukaguzi.

Alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha Baraza la Biashara la Mkoa wa Njombe.

Alisema serikalini kwa sasa kumekuwa na mabadiliko na maboresho mengi kwenye eneo la kodi na elimu ya mlipakodi imekuwa ikitolewa kwa wafanyabiashara nchini.

Alisema makamishna wa TRA wamekuwa wakituma timu kwa ajili ya elimu hiyo, lakini wafanyabiashara wamekuwa wakifunga maduka na kukimbia.

Mtaka alisema serikali ina nia ya dhati ya kuiinua sekta binafsi, hivyo wafanyabiashara wanapoitwa kwenye vikao mbalimbali vinavyowahusu wajitokeze kwa wingi ili kujadili matatizo yao.

"Viongozi wa wafanyabiashara mnaweza kuona utayari wetu sisi serikali kwenye kufunga maduka mnaungana sana lakini mkiitwa kwenye vikao vya kujadili changamoto zenu mnakuja wanne na wengine hamfiki," alisema Mtaka.

Ofisa Biashara Mkoa wa Njombe, Lusungu Mbede, alisema ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe imeanzisha kituo cha pamoja cha utoaji huduma kwa wafanyabiashara ili zipatikane katika eneo moja.

Makamu Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara wa Viwanda na Kilimo (TCCIA) Taifa, Edmund Mkwawa, alisema wafanyabiashara walio wengi wamekuwa wagumu kushiriki vikao pindi wanapoitwa kujadili masuala mbalimbali ambayo yanawatatiza, lakini wanaongoza kwa kutoa malalamiko.

Ofisa Elimu na Mawasiliano kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Njombe, Brian Shoo, alisema mabadiliko ya kodi hufanyika baada ya kukusanya maoni kutoka kwa wadau.

Mmoja ya wafanyabiashara mkoani Njombe, Oraph Mhema, alisema vikao vingi vya baraza la biashara vimekuwa vikiimiza ubia kati ya serikali na sekta binafsi, lakini mara nyingi watumishi wa serikali wanapokuwa wakishughulikia mambo yao hawawachukulii kama ni wadau au wabia katika mnyororo wa thamani.

Meneja Miradi wa Taasisi ya CRDB Foundation, Baraka Kiaro, alisema wana programu maalumu ya Imbeju iliyoanzishwa kwa ajili ya kuwezesha wanawake, vijana na makundi maalumu katika jamii hasa kwenye nyanja mbalimbali zinazohusu uchumi.






Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wa sita kushoto) akiwa na Dk. Eunjae Lee, ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya K-FINCO wakionesha hati ya makubaliano ya ushirikiano wa kuimarisha maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini Tanzania. **Habari kamili Uk. 19** **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamu Rais awapa neno vijana kuhusu Dira ya Taifa



**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, (pichani) amewataka vijana kutoa maoni na kuishauri serikali masuala ya kimaendeleo katika mchakato wa utayarishaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

Aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa kongamano la ukusanyaji wa maoni ya wadau kuhusu Dira ya Taifa ya Mwaka 2050.

Alisema hatua ya ukusanyaji maoni ya wananchi kuhusu Dira ya Maendeleo ya Taifa ni jitihada za serikali katika kuhakikisha uandishi wa Dira ya Mwaka 2050 unazingatia na kuakisi maono na matamanio ya Watanzania.

Hemed alisema ni wajibu wa kila Mtanzania kutoa maoni, kuishauri serikali na kubainisha michango yake ili yaweze kutumika katika dira hiyo.

Aidha, alisema Dira ya Mwaka 2025 imekuwa na mafanikio makubwa na ya kuridhisha ikiwa ni pamoja na kulifikisha taifa katika kundi la nchi zenye kipato cha kati cha chini mwaka 2020.

Hivyo alitoa wito kwa wizara zote, taasisi za umma, idara zote zinazojitegemea, sekta binafsi, Watanzania wanaoishi ughaibuni na watakaopata nafasi ya kuchangia katika rasimu ya Dira ya Taifa kuhakikisha wanatoa maoni ya kujenga.

Naye Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Juma Makungu Juma, alisema Dira ya Taifa ya Maendeleo ni takwa la kikatiba inayotoa fursa ya ushirikishwaji wa wananchi wote bila kujali tofauti zao za kisisa, dini, mila na desturi.

Makungu alisema ili taifa liweze kupiga hatua linahitaji mipango madhubuti itokanayo na maoni, ushauri na mapendekezo kutoka kwa wananchi ambayo yataeleza mahitaji yao muhimu kwa miaka 25 ijayo.

# Magharibi 'A' kuunga mkono utunzaji mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'A', Hamida Khamis Mussa, amesema serikali ya wilaya hiyo itaendelea kuunga mkono juhudi za utunzaji wa mazingira, ili kuhakikisha nchi inabaki salama.

Alisema hayo wakati wa uzinduzi wa zoezi la upandaji miti katika shamba la ushirika la 'Maisha Gemu' lililoko Mwaachealale.

Alisema nchi inakabiliwa na changamoto tofauti za uharibifu wa mazingira unaochangiwa na shughuli za kibinadamu zinazoathiri ustawi wa jamii na uchumi, hivyo kila mmoja katika jamii anapaswa kuchukua hatua kukabiliana na madhara yake.

Hamida ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'B' alisema mazingira ni neno pana linalohusiana na vitu vyote vilivyozunguka binadamu kama vile hewa, ardhi, maji.

Alisema katika kuimarisha mazingira wamekuwa wakifanya jitihada katika kupambana na uharibifu wa mazingira kwa ubunifu mkubwa wa nishati mbadala, ambayo haina madhara kwa mazingira na mtumiaji kwa ujumla.

Aidha, alipongeza ushirika huo kwa kuwa wakala wa usambazaji na uuzaji wa nishati mbadala kwa wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kutunza mazingira.

Baadhi ya wananchi walioshiriki katika upandaji wa miti, walitaka serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuendelea kuzalisha miche mingi ya miti hasa ile ambayo imeanza kutoweka.

# Matukio 165 ya ukatili, udhalilishaji yaripotiwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MATUKIO 165 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa visiwani Zanzibar katika kipindi cha Julai mwaka huu, huku idadi ya matukio hayo yakionekana kupungua ikilinganishwa na Juni.

Ofisa kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ahmada Hassan Suleiman, alisema hayo juzi wakati akiwasilisha taarifa ya matukio hayo kwa kipindi cha Julai.

Alisema katika matukio hayo waathirika wengi walikuwa ni wanawake na watoto, kwamba watoto sawa na asilimia 86.1, wanawake sawa na asilimia 10.9 na wanaume ni asilimia 3.0.

Alisema kati ya waathirika 142, wasichana walikuwa 115 sawa na asilimia 81.0 na wavulana walikuwa 27 sawa na asilimia 19.0 ya waathirika wote.

Vilevile alisema idadi ya matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 68, kwamba waathirika 63 walikuwa wasichana na watano ni wanawake.

Alisema matukio ya kulawiti yalikuwa 19, waathirika 18 walikuwa wavulana na mmoja alikuwa mwanaume, huku matukio ya kuingiliwa kinyume na maumbile yalikuwa tisa ambapo waathirika wanane walikuwa wasichana na mmoja mwanaume.

Alisema matukio mengine yaliyoripotiwa ni kutorosha 19, huku waathirika 18 walikuwa wasichana na mmoja mwanamke, shambulio la aibu yalikuwa 29 kati ya hayo 19 walikuwa wasichana, nane wanawake, mmoja mwanaume na mmoja mvulana.

Alisema: "Matukio ya shambulio la kuumiza mwili yalikuwa 21 ambapo waathirika saba walikuwa wasichana, wavulana nane, wanawake watatu na wanaume watatu."

Aidha, alisema kuwa Wilaya ya Magharibi "B" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyingine kwa matukio 52 sawa na asilimia 31.5 ikifuatia Wilaya ya Mjini iliyoripoti matukio 32 sawa na asilimia 19.4.

Alisema Wilaya ya Kaskazini "A" imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuwa ni matatu kwa kila wilaya sawa na asilimia 1.8.

Ahmada alisema idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 5.2 kufikia matukio 165 kipindi cha Julai, 2024 kutoka matukio 174 kwa Juni mwaka huu.

Alisema Wilaya ya Magharibi "B" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ikilinganishwa na wilaya nyingine kwa kuwa na matukio 52 kwa kipindi cha Julai. Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia , Wazee Wanawake na Watoto, Siti Abasi Ali, alisema kuwa licha ya kupungua kwa makosa hayo ndani ya mwezi huu lakini bado jitihada zinahitajika kwa jamii juu ya kuondoa vitendo hivyo.

Alisema kuwa talaka kuwa nyingi ndani ya jamii imesababisha kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji.

# EACOP yatambua nguvu ya vyombo vya habari kuhabarisha

**Na Kulwa Mzee**

MKUU wa Kitengo cha Mawasiliano wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika ya Mashariki (EACOP), Catherine Mbatia, ameahidi kufanya kazi na vyombo vya habari kutokana na nguvu kubwa viliyonayo katika kufikisha taarifa kwa umma kuhusu mambo mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mbatia alisema wataendelea kutoa elimu kwa waandishi wa habari kupitia njia mbalimbali, ikiwamo kutembelea vyumba vya habari vya magazeti, vituo vya redio na televisheni sambamba na kuandaa semina na kutoa taarifa juu ya maendeleo ya mradi huo.

"Uhusiano wetu na vyombo vya habari ni muhimu sana ili wananchi waendelee kupata taarifa kuhusu maendeleo ya mradi huu, wakati mwingine wananchi wanapenda kujua hatua za utekelezaji mradi huu.

"Mbali ya kutumia mitandao ya kijamii kuwafikia, waandishi wa habari pia wanatumiwa kama daraja muhimu la kuwapatia taarifa za mradi huu," alisema.

Kiongozi huyo alisema wananchi wanahitaji matokeo mbalimbali ya mradi, zikiwamo faida za kiuchumi kwa taifa, hivyo wanahitaji kupewa taarifa sahihi kulinganisha na kila hatua ya mradi huo ambao utahusika kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, mkoani Tanga na baadaye kusafirishwa nje ya nchi.

Akizungumza kuhusu maendeleo ya mradi, Mbatia alisema unaendelea vizuri na matarajio ni kumalizika kwa wakati.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali, ikiwamo ufukiaji mabomba ardhini yatakayosaidia kusafirisha mafuta ghafi kutoka Kijiji cha Hoima, Uganda hadi Chongoleani, mkoani Tanga.

Bomba hilo lina urefu wa kilomita 1,443. Kati yake, kilomita 1,147 ziko Tanzania na kilomita nyingine 296 ziko Uganda.

Wanahisa wa mradi huu ni Kampuni ya TotalEnergies inayomiliki asilimia 62, mashirika ya kusimamia nishati Tanzania (TPDC) na UNOC la Uganda yanamiliki hisa asilimia 15 kila moja wakati lile la China (CNOOC) linamiliki asilimia nane ya hisa.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kulia), akiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya CEOrt, David Tarimo (katikati) na Mkuu wa Chuo cha Strathmore University Business School, Dk. Caesar Mwangi, wakati wa mahafali ya nne ya programu ya mafunzo ya uanagenzi ya mkurugenzi mtendaji. Hafla hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ajenda uchumi wa buluu yaundiwa mkakati

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Mudrik Ramadhan Soraga, ameeleza umuhimu wa kuwa na majukwaa yanayokutanisha viongozi wa serikali na wadau wa uchumi ili kujadiliana fursa na kutatua changamoto zinazoibuka.

Vilevile, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) imeeleza dhamira yake ya kuendelea kushirikiana na wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa kupitia huduma zake mbalimbali za kibenki ili kuchochea ukuaji uchumi na mchango wa wadau hao katika kufanikisha ajenda ya Uchumi wa Buluu na uwezeshaji wa maendeleo visiwani Zanzibar.

Dhamira hiyo ilielezwa na Meneja wa benki hiyo Tawi la Zanzibar, Abdul Karim Mkila, alipozungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi, wakati wa Uzinduzi wa Jukwaa la Kimataifa la Wakuu wa Mashirika na Kampuni visiwani Zanzibar.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Mudrik Ramadhan Soraga aliongoza uzinduzi wa jukwaa hilo, hafla ikihudhuriwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Sharif Ali Sharif.

Jukwaa hilo lilikutanisha pamoja viongozi wa kampuni na mashirika kutoka Tanzania, Kenya, Afrika Kusini, Mauritius na mataifa jirani likiwa na lengo la kuimarisha uchumi wa buluu na kuwezesha wafanyabiashara wa ndani. Benki ya NBC ilikuwa miongoni mwa wadhamini muhimu wa jukwaa hilo.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Waziri Soraga, alitoa wito kwa washiriki kuendelea kushirikiana kwa ukaribu zaidi ili kukuza uchumi wa visiwa hivyo husussani kupitia katika sekta za utalii, biashara, uvuvi na ujenzi wa makazi.

"Tukio hili ni nafasi adimu kwa wafanyabiashara, wakuu wa taasisi, na wadau mbalimbali kukutana na kujadili kwa kina masuala muhimu kuhusu uwekezaji na ukuaji wa uchumi.

"Serikali pia tunalitegemea jukwaa hili kama moja ya namna bora zaidi katika kutusaidia kwa kutupatia ushauri kwenye masuala mbalimbali ya kiuchumi ili kuleta maendeleo endelevu na jumuishi," alisema Waziri Soraga.

"Waziri Sharif alisisitiza umuhimu wa wakuu wa kampuni kukutana mara kwa mara ili kujadili fursa na changamoto zinazokabili sekta mbalimbali za kiuchumi kwa kuwa mijadala na maoni yao kwa kiasi kikubwa yatasaidia kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kukuza uchumi wa Zanzibar hususani kupitia ajenda ya uchumi wa buluu.

"Kwa ujumla uzinduzi wa jukwaa hili unatarajiwa kuwa chachu ya maendeleo huku ukisaidia kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika sekta za uwekezaji na biashara na kuleta mchango mkubwa kwa ustawi wa uchumi wa Zanzibar," alisema.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Mkila alibainisha umuhimu, nia na mchango wa benki hiyo katika kushirikiana na wafanyabiashara pamoja na wadau mbalimbali visiwani humo ili kuchochea ukuaji uchumi kupitia huduma zake mbalimbali zilizobuniwa mahusussi kwa ajili yao ikiwamo mikopo na huduma za bima.

"Kimsingi ni kwamba NBC tumejizatiti kushirikiana na wadau wote katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Jukumu letu ni kuhakikisha tunawezesha wafanyabiashara wadogo, wa kati, na wakubwa kwa kuwapatia huduma bora za kibenki, mikopo na bima, ili waweze kufanya biashara zao kwa ufanisi zaidi," alisema Mkila.

Aliongeza kuwa benki hiyo itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuwezesha maendeleo ya kiuchumi kwa kuleta ushirikishwaji kifedha kwa wafanyabiashara wa sekta zote.

## Bilioni 600/- kutekeleza afya ya mama na mtoto

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imesema Sh. bilioni 641.3 zitatumika kutekeleza Mpango wa Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto (TMCHIP) kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2023 hadi mwaka 2027, unaolenga masuala mbalimbali ikiwamo lishe na afya ya uzazi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa mkutano wa kutambulisha mpango huo sambamba na tathmini ya mkataba wa lishe.

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) na Serikali ya Tanzania utasaidia kuongeza kasi ya utoaji huduma bora za afya ya uzazi, zikiwamo huduma za dharura na upasuaji kwa wajawazito pamoja na matibabu kwa watoto wachanga.

"Katika mpango huu, afua mbalimbali za afya ya mama na mtoto, zitaboreshwa na kuimarishwa ikiwa ni pamoja huduma za wajawazito kabla na baada ya kujifungua, huduma kwa watoto wachanga, huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana balehe pamoja na utekelezaji afua mbalimbali za lishe," alisema.

Mchengerwa alisisitiza wanafunzi walio katika shule za umma na binafsi wapate chakula huku akieleza kuwa mikoa ya Rukwa na Kigoma iko chini ya asilimia 45 kwenye utoaji huduma hiyo, hivyo kuwataka kuongeza kasi.

Alitaja mikoa mingine ambayo utoaji uko chini ni Katavi, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza na Tabora.

Waziri huyo pia aliagiza uhamasishaji wazazi kutiliwa mkazo katika mikoa yote ili wachangie kikamilifu mpango wa chakula shuleni kwa shule za msingi na sekondari.

Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, alisema serikali itakamilisha Sera ya Chakula na Lishe na kuongeza virutubishi lishe ya watoto shuleni.

Pia alisema kwa kipindi cha miaka mitatu, mageuzi yamepatikana ndani ya sekta ya afya ambapo vituo vya kutokea huduma vimeongezwa kwa zaidi ya asilimia 30.

Alisema vituo hivyo vina teknolojia ya vifaa tiba vya kisasa vinavyomaliza matatizo mengi ya magonjwa ndani ya nchi kulinganishwa na nyuma ambapo watu walikuwa wanakwenda nje ya nchi kutibiwa.

Mwakilishi wa wadau wa maendeleo wanaojihusisha na lishe kutoka Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Patrick Codjia, alisisitiza wataendelea kuunga mkono juhudi za serikali kuboresha eneo hilo kwa faida ya Watanzania.

## HABARI KIMATAIFA

# WFP kuchunguza chanzo uhaba chakula

**KHARTOUM, Sudan**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) linawachunguza maofisa wake wawili wakuu nchini Sudan, kwa tuhuma za udanganyifu na kuficha taarifa kutoka kwa wafadhili wa kimataifa, wakati taifa hilo likikabiliwa na uhaba mkubwa wa chakula.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na shirika la habari la RUTERS, wachunguzi wa WFP wanatafuta kufafanua iwapo wafanyakazi walificha jukumu la Jeshi la Sudan katika kuzuia uwasilishaji wa misaada wakati wa vita ambavyo vimeendelea kwa zaidi ya siku 500.

Maofisa wawili wakuu wa taasisi hiyo wanaolengwa na uchunguzi huo ni Naibu Mkurugenzi wa WFP nchini Sudan, Khalid Osman, aliyesimamishwa kazi na Mohammed Ali, Meneja wa Kanda wa WFP, anayechunguzwa kutokana na kutoweka kwa zaidi ya lita 200,000 za mafuta ya Umoja wa Mataifa (UN) katika Jimbo la White Nile.

Wahudumu kadhaa wa kibinadamu na wanadiplomasia walisema wakati wa uchunguzi kuwa wana wasiwasi kwamba usimamizi mbovu katikati mwa ofisi ya WFP nchini Sudan unaweza kuwa umechangia kushindwa kutoa misaada ya kutosha kwa Wasudani wanaohitaji.

Wafanyakazi wa misaada walisema wametatizika kutoa misaada, katika baadhi ya sehemu kwa sababu ya vikwazo vya vifaa na mapigano.

Pia walisema mamlaka zinazohusishwa na jeshi zilizuia ufikiaji kwa kukataa kutoa vibali vya kusafiri na uidhinishaji, wakati askari wa Msaada wa Haraka (RSF) walipora vifaa vya msaada.

Kulingana na UN, watu milioni 25, au zaidi ya nusu ya Wasudani, wanakabiliwa na hali ya utapiamlo mkali. Na Agosti, njaa ilitangazwa katika kambi ya Zamzam huko Darfur.

***RFI***



Wananchi wakishirikiana na mamlaka ya Gabon, kuadhimisha kumbukumbu ya mwaka wa kwanza wa kuondolewa madarakani Rais Ali Bongo. **PICHA: MTANDAO**

# NMB kushirikiana kimkakati na K-FINCO ya Korea Kusini

**SEOUL, KOREA**

BENKI ya NMB imetia saini Mkataba wa Makubaliano (MoU) kushirikiana na shirika la Korea Kusini linalojihusisha na kufadhili miradi katika sekta ya ujenzi la Korea Finance for Construction (K-FINCO).

Lengo la makubaliano hayo ni kusaidia kuwezesha makandarasi wa Korea Kusini kushiriki kikamilifu katika miradi ya ujenzi nchini ambayo NMB itaiwakilisha K-FINCO kwa kutoa dhamana za kupata zabuni za kutekeleza miradi hiyo.

Hafla ya utiaji saini ya ushirikiano huo iliyofanyika Agosti 28 mwaka huu, ilishuhudiwa na Balozi wa Tanzania Korea Kusini, Togolani Mavura.

Ujumbe wa NMB uliongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Ruth Zaipuna, huku ujumbe wa K-FINCO ukiwa chini ya Dk. Eunjae Lee, ambaye ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa taasisi hiyo na Mwenyekiti wa Bodi yake ya Wakurugenzi.

K-FINCO ni taasisi ya ushirika inayosimamiwa na Wizara ya Ardhi, Miundombinu na Uchukuzi ya Korea Kusini, Inajihusisha na utoaji huduma za dhamana na bima kwa kampuni wanachama katika sekta ya ujenzi ya nchi hiyo.

Mkataba huo ambao unatarajiwa kuimarisha maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini, unazichagiza taasisi hizo za kifedha kufanya kazi kwa karibu zaidi ili kuchangia kikamilifu ukuaji wa uchumi wa Tanzania na jitihada za ujenzi wa taifa.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, Benki ya NMB na K-FINCO zitakuwa na jukumu muhimu la kuvutia miradi mikubwa ya ujenzi itakayosaidia kuboresha maisha ya Watanzania.

Imeelezwa na uongozi wa Benki ya NMB kuwa ushirikiano huu pia unatarajiwa kuendeleza ukuaji wa mitaji, kutengeneza ajira, na kuifanya Tanzania kuwa kigogo wa miundombinu katika ukanda huu.

Alisema hatua hiyo nyeti itaimarisha uhusiano wa kiuchumi na kidiplomasia kati ya Tanzania na Korea Kusini, na kukuza urafiki kati ya wananchi wa mataifa haya mawili.

Akizungumzia makubaliano hayo, Zaipuna alisema; „Nina imani kubwa makubaliano haya yamefanyika wakati muafaka. Matarajio ya uchumi wa Tanzania yanavutia wengi kwa sasa kufuatia utekelezaji sera madhubuti za kiuchumi na mageuzi ya mazingira ya kibiashara, jinsi uchumi ulivyoimarika baada ya janga la UVIKO-19 pamoja na dhamira ya taifa ya kuwa na maendeleo makubwa ya miundombinu.

„Baada ya kutia saini MoU hii, tunataka kuona kuendelea kwa juhudi za pamoja za kujenga ushirikiano wa muda mrefu na wa kimkakati kati ya Benki ya NMB na K-FINCO.

„Tunataka kutumia mkataba huu ili kuendeleza zaidi ahadi na matamanio yetu ya maendeleo jumuishi na endelevu ya kijamii na kiuchumi."

Zaipuna aliwashukuru Balozi Mavura na Dk. Lee kwa kuchangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha makubaliano hayo.

Aliwaahidi kuwa Benki ya NMB itafanya kila linalowezekana kuhakikisha malengo ya mkataba huo yanatimia na matokeo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

NMB ni benki ya biashara iliyosajiliwa nchini ikiwa na idara zake kuu tatu ambazo ni ya wateja wadogo au rejareja, wateja wakubwa na Hazina. Benki hiyo pia inahudumia wateja wadogo, wakulima, kampuni ndogo na za kati (SME), kampuni kubwa, taasisi na serikali.

# Museveni aunga mkono uhusiano China na Afrika

**KAMPALA, Uganda**

MARAIS wa nchi za Afrika wakiongozwa na wa Uganda, Yoweri Museveni wamesema kampeni ya vyombo vya habari inayojulikana kama (Washirika wa Afrika) iliyoandaliwa na China Media Group (CMG) itakuza mahusiano ya vyombo vya habari kati ya China na Afrika.

Pia ilielezwa kuwa uhusiano huo utasaidia kuimarisha ushirikiano kwa vitendo baina yao, pamoja na kuchochea mabadilishano ya kiutamaduni na mafunzo ya pamoja katika zama za kidigitali.

Tukio hilo, limetumika katika kusaidia shughuli kwa ajili ya mkutano wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na AFrika (FOCAC), likilenga kuimarisha mabadilishano ya vyombo vya habari na ushirikiano kati ya mataifa hayo.

Rais Museveni alisema, kwa kuwa China ni rafiki wa Afrika anaunga mkono mkutano wa vyombo vya habari unaofanyika Beijing.



"Nawatuma vijana wetu, nataka nao wahusishwe. Unajua, hakuna kitu ambacho sikijui kuhusu China, na wao wanatufahamu sisi pia, lakini nataka vijana kuungana na nyinyi vijana wenzao," alisema.

Aidha, marais kadhaa wa Afrika pia walielezea azma yao ya kuimarisha mabadilishano ya habari kati ya China na Afrika na kuamrisha ushirikiano kwa vitendo katika ujumbe wao kwa njia ya video kwenye tukio hilo.

***VOA***

# Mchakato uchaguzi kuonyesha mustakabali wa kisiasa Ujerumani

**THURINGIA, Ujerumani**

MAJIMBO mawili ya mashariki mwa Ujerumani,Thuringia na Saxony yanapiga kura katika uchaguzi muhimu unaoweza kuonesha mustakabali wa kisiasa wa nchi hiyo.

Ilielezwa kuwa vituo vya kupiga kura vilifunguliwa saa 2:00 asubuhi kwa saa za Ujerumani na kufungwa 12:00 jioni. Na kwamba uchaguzi huo wa bunge wa majimbo huenda ukaonesha mwelekeo wa mitazamo ya Wajerumani kisiasa katika uchaguzi mkuu ujao kitaifa.

Ilielezwa kuwa kiasi kikubwa kinachotazamwa ni kwa namna gani chama cha siasa kali za mrengo wa kulia cha AfD ambacho huenda kinaweza kuwa chenye nguvu katika uchaguzi wa majimbo kwa mara ya kwanza, kitaungwa mkono kwenye uchaguzi huo.

Wachambuzi wa siasa walieleza kuwa inaonyesha kwamba vyama vitatu vilivyomo kwenye serikali ya mseto inayopoteza umaarufu kitaifa inayoongozwa na Kansela Olaf Scholz inaelekea kupata matokeo mabaya zaidi katika uchaguzi huu wa majimbo.

Pia walieleza kuwa huenda matokeo hayo yakazidi kuleta migawanyiko miongoni mwa viongozi hao wakati ukiwa umebakia mwaka mmoja tu ufanyike uchaguzi wa bunge kitaifa.

Uchaguzi mkuu wa bunge nchini Ujerumani utafanyika Septemba 2025. Kabla ya uchaguzi huu wa Thuringia na Saxony, zilifanyika kura za maoni hivi karibuni ambazo zimeonesha chama cha AfD kitapata ushindi wa wazi katika jimbo la Thuringia na karibu na chama cha siasa za wastani za mrengo wa kulia cha Christian Democratic CDU.

Shirika la ujasusi nchini Ujerumani, limekiorodhesha chama cha AfD katika majimbo ya Thuringia na Saxony kuwa chama cha itikadi kali za mrengo wa kulia na limekuwa likichunguza chama hicho kama kundi linaloshukiwa kuwa la itikadi kali kote katika jimbo la Brandenburg na ngazi ya kitaifa.

Kiongozi wa chama hicho katika jimbo la Thuringia, Björn Höcke aliyekuwa mwalimu wa historia alikutwa na hatia mara mbili mwaka huu kwa kutumia nembo ya Manazi iliyopigwa marufuku na alipigwa faini. Na bado anakabiliwa na kesi nyingine ya kuhusishwa na uchochezi.

***DW***

# KMC yaitafutia pumzi Singida Black Stars

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata sare ya bao 1-1 kwenye uwanja wake wa nyumbani dhidi ya Coastal Union Jumatano iliyopita, Klabu ya KMC imesema imeanza maandalizi kwa ajili ya mchezo wake unaofuata dhidi ya Singida Black Stars kwa kucheza mechi kadhaa za kirafiki.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Khalid Chukuchuku, alisema pamoja na kwamba mechi hiyo itachezwa Septemba 12, mwaka huu, lakini tayari wameshaanza maandalizi kwa kucheza mechi moja ya kirafiki na huenda wakacheza zingine ili kuendelea kuwafanya wachezaji wao wasipoteze utimamu wa mwili.

"Malengo yetu na macho yote yapo katika mchezo wetu dhidi ya Singida Black Stars utakaochezwa Uwanja wa Liti, Septemba 12, maandalizi ya mchezo huo yameshaanza na baada ya kucheza dhidi ya Coastal Union, tutacheza mchezo mmoja wa kirafiki, na huenda tukacheza michezo mingine, hii ni kuwafanya wachezaji kubaki na viwango vyao kabla ya mchezo huo wa ugenini ambao utakuwa mgumu," alisema Chukuchuku.

Akiizungumzia timu yao kuanza ligi kwa sare nyumbani, Ofisa Habari huyo alisema ingawa walitarajia kupata ushindi ili waanze ligi vizuri, lakini haijawaondoa kwenye malengo kwani hata msimu uliopita walianza hivyo, lakini wakamaliza nafasi ya tano, ambapo walikuwa wakiiwania nafasi ya nne na Coastal Union.

"Hata msimu uliopita tulianza kama hivi kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo ugenini, halafu tukafungwa mabao 5-0 na Yanga katika mchezo wa pili, lakini baada ya hapo tulicheza mechi zaidi ya sita bila kupoteza, kwa hiyo sare hii tuliyoipata haiwezi kutufanya tuanze kuhaha, ni hali ya mchezo," alisema.

Timu hiyo imecheza mechi moja tu mpaka sasa na ipo nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi moja.

Kwa sasa Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha michuano ya kimataifa, ambapo kuanzia Jumatano ijayo mataifa mbalimbali ya Afrika yatakuwa mzigoni kusaka tiketi ya kucheza fainali za AFCON mwakani nchini Morocco.

# UTEPE LIGI KUU ZANZIBAR 2024/25 KUKATWA IJUMAA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BODI ya Ligi ya Shirikisho la Soka Zanzibar, imetangaza ratiba ya Ligi Kuu visiwani hapa ambayo itaanza kutimua vumbi lake mapema Ijumaa wiki hii.

Ratiba hiyo iliyotangazwa jana ni ya nusu msimu ambayo itatamatika Desemba 16, mwaka huu kwa timu zote 16 kucheza michezo 15 ya mzunguko wa kwanza.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, timu zitakazokata utepe siku hiyo ni Mabingwa Watetezi, JKU SC dhidi ya Wanagenzi Inter Zanzibar, ambao wamepanda daraja msimu huu, mchezo utakaochezwa katika dimba la New Amaan Complex.

Jumamosi wiki hii itakuwa kati ya Mlandege FC na Chipukizi FC katika dimba hilo la New Amaan Complex, wakati kule Gombani Mwenge FC watapepetana na KVZ FC.

Jumapili Wanagenzi Muembe Makumbi City, watavaana na New City katika Uwanja wa New Amaan Complex wakati kule Gombani Tekeleza FC watawakaribisha Kipanga FC.

Septemba 9, mwaka huu, Mafunzo SC watavaana na KMKM SC katika viwanja vya Amaan nje ‚Annex B' wakati Gombani wanajeshi wa Uhamiaji FC watawavaa Junguni FC.

Mechi hizo za mzunguko wa kwanza zitakamilishwa kwa mchezo wa nane kwa timu ya Malindi SC kucheza na Zimamoto SC katika Uwanja wa Amaan nje ‚Annex B' ambapo michezo yote itachezwa saa kumi alasiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Issa Kassim, alisema maandalizi yote ya kuanza msimu mpya wa ligi yamekamilika.

Alisema kwa msimu huu viwanja vitakavyotumika ni New Amaan Complex pamoja na Gombani Kisiwani Pemba.

Hata hivyo, alisema licha ya mabadiliko hayo ya uwanja, lakini pia kutakuwa na ongezeko la idadi ya waamuzi watakaosimamia mchezo mmoja kutoka waamuzi watano na kuwa sita ambaye atakuwa ‚mtathmini wa mechi'.




Kikosi cha wachezaji wa timu ya mpira wa miguu ya wanawake ya Jambe Queens kutoka Kata ya Kicheba wilayani Muheza, Tanga kikiwa pamoja na viongozi wao juzi kwenye fainali ya Bonanza la Muheza Queens Soccer lililofanyika Uwanjani wa Shule ya Sekondari ya Wazazi ya Mbaramo. Bonanza hilo lililodhaminiwa na Ofisi ya Utamaduni, Sanaa na Michezo wilayani Muheza na kushirikisha timu nne; Jambe Queens, Songa Queens, Sega Queens na Economy Queens ambazo zote zimepata zawadi ya mipira lengo likiwa ni kuinua vipaji. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wachezaji 9 Ligi Kuu kuibeba Mtibwa Sugar

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mtibwa Sugar imetangaza kusajili wachezaji wapya tisa, watakaoichezea timu hiyo kwenye Ligi cha Championship inayotarajia kuanza kutimua vumbi, Septemba 15, mwaka huu.

Katika kinachoonekana kuwa wamedhamiria kurejea msimu ujao, klabu hiyo imesajili wachezaji tisa ambao wana uzoefu na mikiki ya Ligi Kuu.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thobias Kifaru, alisema jana kuwa anaamini kwa wachezaji waliowasajili watairejesha Ligi Kuu kwa kishindo msimu ujao.

"Tumefanya usajili mkubwa, tuna wachezaji tisa ambao ni wazoefu wa Ligi Kuu na wengine walipita na kuichezea timu hii misimu kadhaa iliyopita wamerejea tena," alisema.

Wachezaji wapya waliotangazwa kusajiliwa ni Anuari Jabir aliyewahi kuzichezea Klabu za Kagera Sugar na Dodoma Jiji, Amani Kyata akitokea Namungo, Raizin Hafidh (Dodoma Jiji), golikipa, Costantine Malimi (Geita Gold), Erick Kyaruzi pia kutoka Geita Gold, golikipa Benedict Tinoco ambaye alishawahi kuichezea timu hiyo misimu kadhaa nyuma, akiwa pia ameichezea Yanga, Issa Rashid ‚Baba Ubaya' beki wa pembeni wa zamani wa timu hiyo na Simba, na Rajab Mgalula.

Mtibwa ilishuka daraja msimu uliomalizika, ambapo inakwenda kucheza ligi itakayokuwa ngumu msimu huu kutokana na idadi ya timu nyingi zilizowahi kucheza Ligi Kuu kwa misimu tofauti kama Mbeya Kwanza, Biashara United, Geita Gold, Stand United, Polisi Tanzania, Mwadui, African Sports na Mbeya City.

## ZISIKUPITE

### STERLING ALIIKATAA SAUDIA

WINGA wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 29, alikataa ofa ya mshahara wa pauni 650,000 kwa wiki kutoka Saudi Arabia ili kujiunga na Arsenal kwa mkopo kutoka Chelsea. ***(Mirror)***

### TRIPPIER ATUA EYUPSPOR

MLINZI wa Newcastle United mwenye umri wa miaka 33, Kieran Trippier, ambaye alistaafu kuichezea England wiki iliyopita, amekubali mkataba na Klabu ya Eyupspor ya Uturuki. ***(Sportsdigitalal)***

### CHILWELL KWA MKOPO

BEKI wa Chelsea na England, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 27, amepewa ofa ya kuwa mchezaji wa mkopo wa Fenerbahce inayonolewa na Jose Mourinho. ***(Givemesport)***

### ERIKSEN AIVUTIA ANDERLECHT

TIMU ya Ubelgiji ya Anderlecht inavutiwa na kiungo wa kati wa Manchester United na Denmark, Christian Eriksen, 32. ***(Het Belang van Limburg)***

### GUNDOGAN MWAKA MMOJA

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Mjerumani Ilkay Gundogan mwenye umri wa miaka 33, ana chaguo la kuongeza mkataba wake kwa mwaka mmoja hadi msimu mwingine iwapo atajumuishwa katika zaidi ya asilimia 50 ya mechi za City za msimu wa 2024-25. ***(Star)***

### OSIMHEN KUSUGUA NAPOLI

MSHAMBULIAJI wa Napoli, Victor Osimhen, ambaye alilengwa na Chelsea katika dirisha la majira ya kiangazi, ameachwa nje ya orodha ya kikosi cha timu yake kwa msimu wa Serie A. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### LIVERPOOL KUSAJILI KIUNGO

LIVERPOOL inataka kumsajili kiungo mkabaji Januari baada ya kushindwa kusajili katika dirisha la usajili la majira ya kiangazi. ***(Football Insider)***

### ELANGA ALIKATALIWA

KLABU ya Nottingham Forest ilikataa ofa yenye thamani ya pauni milioni 50 kutoka kwa Newcastle United kwa ajili ya winga wa Sweden, Anthony Elanga mwenye umri wa miaka 22, siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho. ***(Sky Sports}***

### REKIK KUTIMKA ARSENAL

MLINZI wa kati wa Arsenal, Mholanzi Omar Rekik mwenye umri wa miaka 22, ambaye hajawahi kuichezea klabu hiyo mechi yoyote ya wakubwa, amekatisha mkataba wake. ***(Fabrizio Romano)***

### GUEHI ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inaweza kumnunua beki wa kati wa Crystal Palace na England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24, msimu ujao wa majira ya joto, wakati atakuwa amebakisha mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake. Guehi alikuwa akilengwa na Newcastle United katika dirisha la usajili msimu huu. ***(Mirror)***

### MAN ILIKATAA

KLABU ya Manchester United ilikataa ombi la mkopo kutoka kwa Real Betis kwa winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, na kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen (32), siku ya mwisho ya usajili. ***(Mail)***

## DOND A SOKA MAGAZ A ULAYA



# RAPHINHA ATOA TAMBO BARCA IKIPIGA MTU WIKI

Ni wakati akitupia hat-trick, asema mechi hiyo imeonesha hakuna haja ya wachezaji wapya...

**BARCELONA, Hispania**

RAPHINHA amesema Barcelona walionesha kuwa hawahitaji usajili wowote mpya baada ya kufunga hat-trick katika ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Real Valladolid Jumamosi katika Uwanja wa Olympic kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Barca iliwaleta Dani Olmo na Pau Víctor, mapema msimu huu wa majira ya joto, lakini dirisha la usajili lilifungwa Ijumaa bila ya kuongezwa mchezaji, licha ya kuhusishwa na wachezaji mbalimbali, akiwamo winga wa Athletic Club, Nico Williams, ambaye anacheza katika nafasi ya Raphinha upande wa kushoto.

„Mchezo wa leo (juzi), umeonesha kuwa hakuna haja ya wachezaji wapya kuingia," alisema Raphinha akiwaambia waandishi wa habari baada ya Barca kupata ushindi wa nne katika mechi nne chini ya kocha mpya Hansi Flick kwenye LaLiga msimu huu.

„Tuko katika hali nzuri. Timu inatoa kila kitu katika michezo na mazoezi. Matokeo leo (juzi) yanaonesha tunachofanyia kazi ni kuja pamoja."

Raphinha alitangulia kufunga dhidi ya Valladolid dakika ya 20 akimalizia vema baada ya kudhibiti pasi nzuri ya muda mrefu kutoka kwa beki wa kati Pau Cubarsí.

Robert Lewandowski na Jules Kounde walifanya matokeo kuwa 3-0 kabla ya mapumziko, huku Raphinha akikamilisha hat-trick yake kipindi cha pili kabla ya mabao ya dakika za lala salama kutoka kwa Olmo na Ferran Torres kuhitimisha ushindi.

„Sijui kama ulikuwa uchezaji wangu bora zaidi, lakini hakika mmoja wao," alisema mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil kuhusu kiwango chache, ambapo pia alijumuisha pasi ya bao la mwisho la Torres.

"Nina furaha sana. Ni hat-trick yangu ya kwanza kabisa. Nina furaha kusaidia timu kupata ushindi. Najisikia vizuri. Nimekuwa nikifanya kazi kwa bidii tangu nirudi kutoka likizo.

"Nilijua huu ungekuwa msimu muhimu sana kwangu na ninataka kuwa katika ubora wangu kusaidia wachezaji wenzangu."

Kocha wa Barca, Flick alisema anatumaini haitakuwa mara ya kwanza kwa hat-trick ya Raphinha kwani kuna nyingine zinakuja, huku pia akisifu uthabiti wa safu yake ya ushambuliaji.

"Nadhani Raphinha ana ubora wa kufanya hivyo mara kwa mara," alisema Flick katika mkutano na wanahabari. „Alikuwa na uchezaji mzuri. Nadhani anajisikia huru zaidi uwanjani hivi sasa.

"Kwetu sisi ni muhimu akihamia nafasi nyingine, mchezaji mwingine ana jukumu la kwenda katika nafasi aliyo kawaida, tunafanya mambo mengi kuwa mazuri sana, Rapha ni mmoja wa wachezaji katika mechi nne zilizopita ambao walifanya kweli."

Ushindi huo uliendeleza mwanzo mzuri wa Flick kama bosi wa Barca baada ya kuchukua nafasi ya Xavi Hernandez mapema msimu huu wa majira ya joto, ukija baada ya ushindi dhidi ya Valencia, Athletic Club na Rayo Vallecano.

‚The Blaugrana' ndio timu pekee kwenye LaLiga iliyo na rekodi ya kushinda kwa asilimia 100, lakini Flick anajua mambo yanaweza kubadilika haraka kuelekea mapumziko ya kwanza ya kimataifa ya msimu huu.

"Jambo bora zaidi ni kwamba timu ilicheza tangu mwanzo jinsi tulivyotaka, hiyo ilikuwa nzuri sana," alisema Mjerumani huyo.

„Tulisema tunapaswa kuwa fiti kwa asilimia 100 kutoka filimbi ya mwamuzi na tulikuwa wazuri, tukitengeneza nafasi tangu mwanzo na kushinikiza.

"Unapohisi jinsi mashabiki wanavyotuunga mkono uwanjani, wanaweza kuhisi kulikuwa na kitu cha kipekee leo (juzi) uwanjani.

„Timu ina njaa, baada ya kila bao, kwenda kwa lingine. Na nguvu haikushuka baada ya dakika 85, 90. Ni nzuri. Pia ndio inawafanya mashabiki wajivunie.

"Inanifanya nijivunie, lakini ni mechi ya nne tu, najua inaweza kubadilika kwa kasi sana, msimu ni mrefu sana, lakini bila shaka ni nzuri kwa sababu mashabiki wana furaha.

„Hiki ndicho tunachotaka kufanya na kazi yetu, lakini tuna safari ndefu hadi mwisho wa msimu. Tunataka kujaribu kufanya kila mechi kuwa bora zaidi."




# HAALAND HAZUILIKI EPL - GUARDIOLA

**LONDON,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, alimtaja Erling Haaland kuwa "hawezi kuzuilika" baada ya mshambuliaji huyo kufunga hat-trick ya pili mfululizo na kuweka rekodi mpya ya kufunga mabao mengi katika mechi tatu za kwanza msimu mpya wa Ligi Kuu England, EPL.

Baada ya ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Ipswich Town wiki moja iliyopita, Haaland alikuwa sawa tena akiwa na mabao matatu ya City katika ushindi wao wa 3-1 dhidi ya West Ham Jumamosi na kufikisha idadi yake ya mabao saba.

Bao la kwanza la Haaland lilikuwa ni mchezo mzuri uliompita Alphonse Areola baada ya Bernardo Silva kumchezesha moja kwa moja, huku la pili lilikuwa ni shuti la umbali mrefu.

Na Guardiola alisema anafikiri mabeki hawawezi kumzuia Haaland hata kwa hatua kali.

"Bao la kwanza, Bernardo anashinda mpira, pasi mpira na kumaliza au bao la tatu, na nafasi nyuma, haiwezi kuzuilika," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Hakuna mlinzi wa kati, hata kwa bunduki - haiwezekani kumzuia."

Mchezaji huyo wa Norway mwenye umri wa miaka 24, hiyo ilikuwa ni hat-trick ya 11 kwa City pia ilimaanisha kuwa mchezaji wa pili katika historia ya Ligi Kuu ya England, pamoja na Harry Kane, kufunga hat-trick mara mbili katika mechi mfululizo.

Guardiola alisema Haaland alitatizika msimu uliopita, wakati bado alikuwa mfungaji bora wa ligi akiwa na mabao 27, na sasa alikuwa mchezaji bora zaidi.

Haaland, ambaye alirekodi bao lake la 70 la Ligi Kuu katika mchezo wake wa 69, alisema anahisi manufaa ya kupumzika.

"Ninajisikia vizuri, najisikia nguvu," aliiambia Sky Sports. "Nilikuwa na likizo ndefu na maandalizi ya msimu. Najisikia vizuri.

"Miaka ambayo nimekuwa hapa imekuwa ya haraka sana. Sasa nimepata mapumziko katika mwili wangu na miguu yangu. Sasa niko tayari kwa zaidi."

## Arteta akerwa kadi nyekundu ya Rice

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amekiri "nilishangazwa" na uamuzi wa kumtoa Declan Rice katika mchezo wa Arsenal wa sare ya bao 1-1 dhidi ya Brighton & Hove Albion kwenye Ligi Kuu England, juzi.

Huku 'Washikabunduki' hao wakiwa mbele kwa bao 1-0 wakati huo, Rice alioneshwa kadi ya pili ya njano kwa kuubutua mpira kwa hasira, na uamuzi huo hatimaye ukabadilisha mchezo na kumruhusu Joao Pedro kufunga bao la kusawazisha muda mfupi baadaye.

Pedro labda alibahatika kuepuka hali kama hiyo. Alipiga mpira nje baada ya kutoa mpira wa kurushwa katika kipindi cha kwanza lakini akaepuka adhabu, kumaanisha kuwa kadi yake ya njano.

Alipoulizwa mawazo yake baada ya mchezo huo, Arteta awali alidai kuwa Rice, ambaye aliuwahi mpira bila kukusudia kabla ya kujaribu kuupiga, hakuchelewesha muda kwa makusudi, ambayo ndiyo sababu rasmi iliyomfanya aoneshwe kadi ya pili ya njano.

"Nilishangaa," alisema. "Anashangaa, anashangaa, anashangaa. Mpira unapiga kisigino cha Declan, haoni mchezaji. Katika kiwango hiki, kwa uaminifu ninashangaa."

Baadaye, Arteta alimkosoa mwamuzi Chris Kavanagh kwa kushindwa kumuonya Pedro katika kipindi cha kwanza.

"Katika kipindi cha kwanza wakati wapinzani walifanya hivyo hawakupata kadi yoyote," alisema bosi huyo wa Arsenal akiiambia MOTD.

"Anatoa wito kwa sheria katika eneo lisilo la muhimu la uwanja wakati mpira ukigonga kisigino wakati wa kugeuka, kufanya uamuzi huo ... kwa sheria anaweza kufanya hivyo, lakini kuwa na msimamo.

"Inashangaza, timu na mwitikio wa umati baada ya kumtoa mtu chini. Tulitengeneza nafasi mbili kubwa moja dhidi ya moja na tulipaswa kushinda mchezo."

## Klabu Ulaya zamlilia Sol Bamba

**ISTANBUL,** Uturuki

MLINZI wa zamani wa Ivory Coast, Sol Bamba, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 39, Klabu ya Adanaspor ya Uturuki, ambako alikuwa mkurugenzi wa ufundi, ilitangaza jana.

Bamba alichezea Cardiff City, Leeds United na Leicester City. Pia aliwahi kuichezea Palermo ya Italia, Klabu za Scotland za Dunfermline Athletic na Hibernian, na Trabzonspor ya Uturuki.

Aliichezea nchi yake mechi 46, akifunga bao moja na akastaafu Januari 2023, kisha akaenda kufundisha, akihudumu kama kocha msaidizi huko Cardiff kabla ya kuchukua nafasi ya mkurugenzi wa kiufundi huko Adanaspor.

"Mkurugenzi wetu wa ufundi Souleymane Bamba, ambaye aliugua kabla ya mechi ya jana dhidi ya Klabu ya soka ya Manisa, alipelekwa katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Manisa Celal Bayar na kwa huzuni alipoteza vita vyake vya maisha," ilisema taarifa ya Adanaspor.

"Rambirambi zetu ziende kwa familia yake na jamii yetu."

Cardiff City, ambapo Bamba alipanda nayo Ligi Kuu England katika msimu wake wa kwanza, ilitaja mchango wake kwa klabu hiyo 'kutoweza kupimika.'

"Ni kwa masikitiko makubwa kwamba tumejifunza jioni ya leo kuhusu kifo cha nguli wa Klabu, Sol Bamba. Alikuwa shujaa wetu sote, kiongozi katika kila chumba cha kubadilishia nguo na muungwana wa kweli," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

"Hizi ni habari za kusikitisha kabisa. Sol Bamba ameaga dunia akiwa na umri wa miaka 39, pekee. Tunatuma rambirambi zetu kwa familia," taarifa ya Timu ya Taifa ya Ivory Coast, ilisema kwenye Instagram.

Leeds United walimwita 'mmoja wa watu wazuri zaidi katika soka.'

"Mawazo ya kila mtu katika Leeds United yako pamoja na familia na marafiki wa Sol katika wakati huu wa huzuni. Pumzika kwa amani Sol, utakuwa milele mioyoni mwetu,' klabu ilisema katika taarifa yake.



HABARI MICHEZO

# KCB YASHIRIKI MBIO NA KUCHANGIA MILIONI 30/-

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inaendelea kuunga mkono shughuli za kijamii na miradi ya taasisi mbalimbali ili kukuza kuleta maendeleo nchini, Benki ya KCB imeshiriki mbio maalum kwenye sherehe za shukrani za Marian Schools, zilizojumuisha mbio, matembezi na misa ya shukrani na kuchangia Sh. milioni 30.

Sherehe, mbio na matembezi hayo ambayo yalifanyika shuleni hapo wiki iliyopita, mbali na mgeni rasmi ambaye alikuwa Mkurugenzi wa Biashara wa Kanda wa KCB Group na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo nchini, Cosmas Kimario, pia ilihudhuriwa na wageni mbalimbali wakiwamo Askofu Mkuu wa Shirika la Roho Mtakatifu Zanzibar, Agustine Shao na Mkuu wa Shirika la Holy Ghost, Shauri Selenda.

Wengine waliohudhuria na kushiriki matembezi hayo ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Meneja na Mwanzilishi wa Taasisi za Marian, Fr. Valentine Bayo, viongozi na wafanyakazi wa Benbi ya KCB; Mapadri wa Shirika la Roho Mtakatifu; wenyeviti wa bodi za Taasisi za Marian, pamoja na wazazi, wanafunzi, na wafanyakazi wa taasisi hizo.

Akizungumza baada ya mbio na matembezi hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB Tanzania, Kimario alizipongeza Taasisi za Marian kwa mafanikio makubwa zilizofikia kielimu, kijamii na kiuchumi.

Kimario alisisitiza kuwa tangu kuanzishwa kwa Taasisi za Marian mwaka 1997, zimeonesha dhamira thabiti ya kutoa elimu bora na kuzalisha wahitimu wenye mchango mkubwa katika jamii na tija kazini.

Mkurugenzi huyo aliendelea kwa kueleza jinsi Marian ilivyopanua shughuli zake kutoka shule moja, ya Sekondari ya Wasichana ya Marian (Marian Girls Secondary School), hadi kuwa na shule tatu za sekondari, zahanati, hoteli, na chuo kikuu (Marian University), kilichoanzishwa mwaka 2014.

„Mafanikio haya yameleta mabadiliko chanya katika elimu, jamii, na uchumi wa taifa. Wahitimu wa Marian Schools wameiva kielimu na kinidhamu, wakitoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa," alisema.

Naye Fr. Valentine Bayo, Meneja wa Shule za Marian, alitoa historia fupi ya Taasisi za Marian, akisema: „Mnamo mwaka 1991 nilitumwa hapa na wakubwa wangu wa Shirika la Roho Mtakatifu (Holy Ghost Fathers) kama padre kijana kwa kazi ya uinjilishaji.

„Kutokana na hali ya uduni wa eneo hili ambalo lilikuwa limesahaulika, tulianzisha juhudi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuanzisha shule za chekechea na ufundi. Hatimaye, juhudi hizi zilisababisha kujengwa shule ya sekondari ya wasichana ya Marian mnamo mwaka 1997. Tangu kuanzishwa kwake, shule hii imekuwa kielelezo cha mafanikio nchi nzima na kusaidia uanzishwaji wa taasisi nyingine za Marian kama zifuatazo," alisema.

Alizitaja taasisi hizo kuwa ni Shule ya Awali na ya Msingi ya Marian (Marian Pre and Primary School) Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Marian - Kerege (Marian Boys Secondary School - Kerege), Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Mlingotini (Marian Boys Secondary School - Mlingotini), Shule ya Marian Mater Dei (Marian Mater Dei Girls Secondary School), Stella Maris Hotel, Marian Aggregates and Concretes Lt na Marian Farms.

Kati ya mwaka 2021 na 2024, KCB Bank imewekeza katika miradi mbalimbali ya Taasisi za Marian, ikiwa ni pamoja na ukarabati wa shule za Wasichana za Marian za msingi, ujenzi wa majengo ya ghorofa sita kwa ajili ya madarasa na hosteli za Marian wavulana, na kuchangia baadhi ya gharama za uendeshaji wa taasisi hizo.



Wadau, viongozi mbalimbali wa Benki ya KCB na wafanyakazi wa Taasisi za Marian, wakifanya matembezi wakati wa mbio maalum kwenye sherehe za shukrani za Marian Schools, zilizofanyika shuleni hapo wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

# Mabao kiduchu raundi ya kwanza msimu huu

**Na Adam Fungamwango**

MABAO 14 tu yamefungwa katika mechi za raundi ya kwanza msimu huu, ikiwa ni machache kuliko yaliyofungwa raundi hiyo msimu uliopita.

Mabao hayo yamefungwa katika mechi nane baada ya timu zote kucheza mchezo mmoja wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Msimu uliopita jumla ya mabao 22 yalifungwa katika mechi za raundi ya kwanza kwa timu zote 16 kucheza mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu, hivyo kuwa na pungufu ya mabao manane.

Mechi za raundi ya kwanza msimu huu ulioanza Agosti 16, mwaka huu, zilihitimika kwa Mashujaa FC Kuidungua Dodoma Jiji bao 1-0, KenGold ikazabuliwa mabao 3-1 dhidi ya Singida Black Stars, Simba ikairarua Tabora United mabao 3-0, JKT Tanzania na Azam FC zikatoka suluhu, KMC na Coastal zinatoka sare ya bao 1-1, na Yanga ikaichapa Kagera Sugar mabao 2-0 na Namungo ikaata kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Fountain Gate.

Msimu uliopita, Ligi Kuu Tanzania Bara ilianza kwa Geita Gold kushinda bao 1-0 dhidi ya Ihefu, JKT Tanzania kuichapa Namungo bao 1-0, Dodoma Jiji ikichapa Coastal Union mabao 2-1, Mashujaa ikashinda 2-1 dhidi ya Kagera Sugar, Azam ikaibabua Tabora United mabao 4-0, Simba ikashinda 3-2 dhidi ya Mtibwa Sugar, Singida Fountain Gate na Prisons zikatoka suluhu na Yanga ikapata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya KMC.

Tayari msimu huu mechi tano za raundi ya pili zimechezwa, ambapo ukijumlisha na mechi za nane za raundi ya kwanza, jumla ya michezo 13 inakuwa imeshakamilika, huku ligi hiyo ikisimama kupisha mechi za kimataifa ambapo timu za taifa zitakuwa kibaruani kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025, zinatazofanyika nchini Morocco.

Mpaka sasa jumla ya mabao 22 yamefungwa na wachezaji 21, ambapo straika wa Simba, Valentino Mashaka ndiye pekee aliyefunga mawili. Katika michezo hiyo, tayari penalti nne zimeshatolewa na tatu zimewekwa ndani ya wavu, moja ikiota mbawa, timu tano zilishinda ugenini, tatu nyumbani na sare tano.

# Ibenge: Simba ni Simba tu, itatisha

INATOKA UK. 24

ezo wa wachezaji wa pande zote mbili, utimamu wao wa mwili na kasi ni tofauti na mechi za Ligi Kuu nilizoziona," alisema.

Alisema alichokipata na kujifunza yeye na wachezaji wake ni kutumia nafasi chache wanazozipata ili kuua mchezo.

"Niliwaonya wachezaji wangu vyumbani kwa sababu hawakuimaliza mechi mapema, itakuja kutupa matatizo kipindi cha pili na kweli ikawa hivyo, lakini hii ni mechi ya kirafiki nimetumia wachezaji karibuni wote na kila mmoja amenionesha kitu na kila kitu kitafanyiwa kazi," alisema.

Katika mchezo huo, straika Leonel Ateba alicheza mechi yake ya kwanza na kufunga bao, huku Pokou Serge, raia wa Ivory Coast akipachika bao la kusawazisha.

Wakati Simba inatarajiwa kucheza mechi ya raundi ya kwanza Kombe la Shirikisho dhidi ya Al Ahly Tripoli ya Libya, Al Hilal itacheza raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya San Pedro ya Ivory Coast.

# Gamondi ashtukia wapinzani Ligi Kuu

INATOKA UK. 24

chochote kuhusu mchezo huo kwa sababu wachezaji wake 14 wako kwenye timu za mataifa mbalimbali wakizitumikia kwa ajili ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazotarajia kufanyika mwakani nchini Morocco.


"Sina chochote kwa sasa, ninachoweza kusema ni mkakati wa kiufundi dhidi ya mchezo wetu ujao dhidi ya CBE ni zaidi ya malengo, kwa sababu wachezaji wangu 14 wameondoka kwenda kuzichezea timu zao za taifa, watakaporejea na kuanza mazoezi, ndipo nitakapoweza kusema chochote," alisema.

Yanga itaanzia ugenini, Septemba 13 kwenye Uwanja wa Abebe Bikila nchini Ethiopia, kabla ya mechi ya marudiano kufanyika nchini, Septemba 20, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Michezo
Jumatatu Septemba 2, 2024
Nipashe

## Haaland hazuiliki EPL - Guardiola

UKURASA 22



**TUMENOGA...**




Nyota waliopeleka furaha Simba, Ladack Chasambi, ambaye alimpikia bao, Leonel Ateba, wakipongezana baada ya kuiweka timu yao mbele dhidi Al Hilal Omdurman wakati miamba hiyo ikitoka sare ya 1-1 kwenye mechi ya kimataifa ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa KMC, Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Ibenge: Simba ni Simba tu, itatisha

### ●●● Asifu kupata ushindani mkali, asema linapokuja suala la mechi za CAF ni tishio, Fadlu naye...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Al Hilal Omdurman ya Sudan, Florent Ibenge, amesema Simba ina kikosi kizuri ambacho kinaweza kufanya vema mbele ya safari, huku akiongeza kuwa siku zote hana wasiwasi na timu hiyo inapocheza michezo ya kimataifa.

Akizungumza baada ya mchezo wa kirafiki wa kimataifa uliochezwa jana kwenye Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam, kocha huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alisema japo kwa sasa ipo kwenye maandalizi ya msimu na inakisuka tena upya kikosi chake, lakini ameiona kuwa bado ni timu ngumu na bora itakayoendelea kutisha Afrika, huku akifurahi kupata kipimo kizuri kutoka kwao.

Alisema siku zote huwa hana wasiwasi na Simba hasa linapokuja suala la kucheza michezo ya kimataifa, akisema kwa sababu wanatengeneza timu ni muda ndiyo utaongea.

"Simba ni Simba tu hata iweje, ina kikosi kizuri, na ni moja kati ya timu bora barani Afrika na hapa ipo kwenye maandalizi, hata kama inakwenda kucheza Kombe la Shirikisho, lakini ni timu kubwa sana, unaweza kuiona ya kawaida, lakini kwenye michuano ya kimataifa inakuwa ni nyingine kabisa kama ilivyokuwa leo (Jumamosi) hapa, nimepata kipimo kizuri kwa timu ngumu sana, nadhani ilikuwa ni mechi nzuri ya kipimo kwetu na kwao pia," alisema Ibenge.

Akizungumzia mechi hiyo, alisema nia yake ilikuwa ni kushinda, lakini amekutana na upinzani mkali kama kawaida kutoka kwa Simba.

"Nilikuja hapa kucheza mechi na kushinda, lakini hatujashinda, ila tumefanya kile ambacho tumeweza kukifanya, nawashukuru wachezaji wangu.

"Hatukuanza mechi vizuri, tulicheza nyuma sana, labda waliiogopa Simba, tulifanya makosa mengi kipindi cha kwanza, hatukumiliki mpira, tulikuwa tunaacha mianya mingi, na makosa mengi, tulipoteza pasi pia, lakini, kipindi cha pili nilibadilisha, tulianza vizuri, lakini tukapata kadi nyekundu, bado tukapambana, tukarudisha bao tumetoka sare, siyo mbaya," alisema.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, alionyesha kufurahi kupata ladha halisi ya michuano ya kimataifa yeye na wachezaji wake.

"Nifikiri hiki ni kipimo kizuri, mechi hii ilikuwa na ladha ya mechi za kimataifa za Ligi ya Mabingwa na Shirikisho, katika michezo hii ukiipata nafasi itumie, ukikosa utaadhibiwa, kwa hiyo nimefurahi kupata ladha hii mimi na wachezaji pia, umeona mechi ya leo, uw-

INAENDELEA UK. 23

## Gamondi ashtukia wapinzani Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ametabiri kuwa Ligi Kuu msimu huu, itakuwa ngumu kuliko ya msimu uliopita kwa jinsi alivyoona wapinzani wake, Kagera Sugar, walivyocheza Alhamisi iliyopita katika Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Gamondi alisema inaonekana timu zimejiimarisha kwani wapinzani wao walikuwa wakiwashambulia sana tofauti na inavyokuwa katika michezo mingi ya Ligi Kuu msimu uliopita ambapo timu nyingi zilikuwa zikipaki basi hata kama ziko nyuma kwa mabao 2-0.

Alisema pamoja na kwamba wachezaji wake walikosa mabao mengi kitu ambacho kilisababisha wawape nguvu wapinzani, lakini kitendo cha kushambuliwa mfululizo na wapinzani kimempa somo tosha la kwenda kujiandaa kukabiliana na ugumu wa Ligi Kuu msimu huu.

"Ukiangalia kipindi cha pili, Kagera Sugar walirejea kwa lengo la kurudisha bao, walitushambulia sana, hawakukaa nyuma ili wasifungwe mabao mengi, walitusukuma sana langoni kwetu, lakini tuliweza kuwakabili na kuwadhibiti hadi pale tulipopata bao la pili, hii inaonesha si wao tu, timu nyingi zimejiimarisha sana kwenye Ligi Kuu msimu huu, kwa hiyo ni lazima tujizatiti. Nitarudi kwenye uwanja wa mazoezi kulifanyia kazi, kwa sasa tupo kwenye mapumziko ya Kalenda za FIFA," alisema kocha huyo.

Katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ilishinda mabao 2-0, ya Maxi Nzengeli na Clement Mzize.

Hata hivyo, alisema kwa sasa akili yake kwanza ipo katika mchezo wa raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CBE ya Ethiopia, kwani lengo lake na klabu kwa ujumla ni kufuzu hatua hiyo kabla mengine hayajafuata.

Alisema ni vigumu kwa sasa kusema

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042